# MIELEKEO YA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI KUHUSU METHALI KINZANI; UCHUNGUZI KATIKA KATA YA KITUI MJINI; KAUNTI YA KITUI; KENYA.

**CATHERINE MUTEI MBUSYA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI CHUO KIKUU CHA SOUTH EASTERN KENYA**

**APRILI, 2019**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

Sahihi------------------------------------------ Tarehe----------------

Catherine Mutei Mbusya

**C59/KIT/20638/2015**

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya

**WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii katika chuo kikuu cha South Eastern Kenya.

Sahihi------------------------------------------ Tarehe----------------

Dktr. Esther Njoki Chomba

**Mhadhiri**

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya

Sahihi-------------------------------------------- Tarehe---------------------

Dktr. Musyoka Francis Mwangangi

**Mhadhiri**

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya

## SHUKRANI

Ninachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kwa rehema zake alizonijalia mpaka kuikamilisha kazi hii. Changamoto nilizokabiliana nazo si haba lakini kwa neema zake nimeona tamati ya safari hii ambayo haikuwa rahisi.

Pili, naishukuru familia yangu kwa kusimama nami nilipokuwa nikifanya kazi hii wakati wa kuiandika na wakati wa utafiti. Mume wangu mpendwa Zacharia pokea shukrani tele kwa kunihimiza nimalize utafiti huu. Tumefanikiwa pamoja.

Shukrani zangu maalum ni kwa wasimamizi wangu wawili; Dktr. Esther Chomba na Dktr. Francis Mwangangi. Mlivyonikuza kama wahadhiri na kunielekeza kama wasimamizi wangu katika utafiti huu; Mungu azidi kuwanyeshea mvua ya baraka maishani mwenu. Mhadhiri Bi. Ngesu ulinifunza mengi kuhusu utafiti wa Kiswahili. Baraka za Mungu ziwe nawe siku zote.

Nitakuwa mpungufu wa shukrani iwapo sitawashukuru watafitiwa wote walioshiriki katika zoezi hili. Ushirikiano wenu na usimamizi wa shule nilipowatembelea katika kata ya Kitui mjini ulikuwa wa kuridhisha moyo. Kujitolea kwenu kushiriki katika utafiti huu kumeipa kazi hii ufanisi mkubwa sana.

Shukrani nyingi ziwaendee wazazi kwa malezi bora, ushauri wenu tukiwa pamoja na zaidi maombi yenu kwangu. Kwa hakika mmechangia pakubwa sana katika ufanisi nilio nao maishani. Marafiki zangu Jane Mutunga na Evelyn Muthui pokeeni shukrani za kipekee kwa mapenzi na mawaidha mliyonipa na ambayo yalichangia kukamilika kwa kazi hii. Mungu awabariki.

# TABARUKU

Naitabaruku Tasnifu hii kwa familia yangu; mume wangu mpendwa Zacharia na mtoto wangu Ivanna Kerubo. Mapenzi yangu kwenu hayana kipimo.

# MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **Wanafunzi** | Wanaosoma fasihi ya Kiswahili katika kiwango cha shule za upili, kidato cha tatu na nne |
| **Walimu** | Wanaofundisha fasihi ya Kiswahili katika shule za upili |
| **Paremiolojia** | Taaluma inayoshughulikia methali |
| **Methali** | Semi fupi ya kimapokeo yenye muundo mahsusi na iliyo na Fumbo fupi ambalo linapofasiliwa hupata maana mbalimbali kutegemea muktadha na hali ya maisha ya mtumiaji |
| **Dktr** | Daktari |
| **N.k** | Na kadhalika |
| **SPSS** | *Statistical Package for Social Sciences* |
| **TATAKI** | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |

# YALIYOMO

**IKIRARI** ... ii
**SHUKRANI** ... iii
**TABARUKU** ... iv
**MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUPISHO** ... v
**YALIYOMO** ... vi
**ORODHA YA MAJEDWALI** ... viii
**ORODHA YA MICHORO** ... ix
**IKISIRI** ... xi
**SURA YA KWANZA** ... 1
1.0 Utangulizi ... 1
1.1 Usuli wa Mada ... 1
1.2 Suala la Utafiti ... 4
1.3 Madhumuni ya Utafiti ... 5
1.4 Maswali ya Utafiti ... 6
1.5 Umuhimu wa Utafiti ... 6
1.6 Upeo na Mipaka ... 6
**SURA YA PILI** ... 8
**UDURUSU WA MAANDISHI** ... 8
2.1 Utangulizi ... 8
2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ... 8
2.3 Fasili ya Methali ... 11
2.4 Uainishaji wa Methali ... 12
2.4.1 Kigezo cha Kimaana ... 12
2.4.2 Kigezo cha Kiuamilifu ... 13
2.4.3 Kigezo cha Kimuundo/Kimtindo ... 13
2.4.4 Kigezo cha Kialfabeti ... 13
2.4.5 Kigezo cha Kimuktadha ... 14
2.5 Msingi wa Nadharia ... 14
2.5.1 Nadharia ya mguso ... 14
2.5.2 Nadharia ya umaanishaji ... 15
**SURA YA TATU** ... **17**
**MBINU ZA UTAFITI** ... **17**
3.1 Utangulizi ... 17
3.2 Muundo wa Utafiti ... 17
3.3 Uteuzi wa Sampuli ... 17
3.4 Ukusanyaji wa Data ... 19

3.4.1 Hojaji........................................................................................................ 19
3.4.2 Mbinu ya maktabani ........................................................................................ 19
3.5 Uchanganuzi wa Data ........................................................................................ 19
3.6 Uwasilishaji wa Matokeo..................................................................................... 20
**SURA YA NNE ............................................................................................................ 21**
**UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO .......................... 21**
4.0. Utangulizi.......................................................................................................... 21
4.1. Hojaji zilizojazwa na kurudishwa ......................................................................... 21
4.2 Utangulizi wa Habari za Msingi za Wanafunzi ........................................................ 22
4.3 Ukinzani Unavyojitokeza ndani ya Baadhi ya Jozi za Methali.................................. 23
4.4 Uchanganuzi wa Jozi za Methali za Kiswahili ......................................................... 24
4.5 Umuhimu wa Ukinzani Katika Methali za Kiswahili ................................................ 35
4.6 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Ukinzani Katika Methali za Kiswahili .................... 36
4.7 Uchanganuzi wa Data Kutoka kwa Walimu ............................................................ 38
4.8 Uchanganuzi wa Data Inayohusiana na Mada ya Utafiti ........................................... 43
**SURA YA TANO ......................................................................................................... 53**
**MUKHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO.................................................... 53**
5.1 Utangulizi.......................................................................................................... 53
5.2 Mukhtasari wa Matokeo ..................................................................................... 53
5.3 Hitimisho........................................................................................................... 54
5.4 Mapendekezo ..................................................................................................... 55
**VIAMBATISHO .......................................................................................................... 60**
Kiambatisho I: Hojaji kwa Wanafunzi..................................................................... 60
Kiambatisho II: Hojaji kwa Walimu........................................................................ 64
Kiambatisho III: Ratiba ya Kazi ............................................................................. 67
Kiambatisho IV: Bajeti .......................................................................................... 68
Kiambatanisho III: Orodha ya Shule za Upili Eneo Bunge la Kitui Mjini ................... 69

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1 Orodha ya Shule ambapo Uchunguzi Ulifanywa………………… .........17
Jedwali 4.1 Hojaji zilizojazwa na kurudishwa…………………………...................20
Jedwali 4.2 Jinsia ya mtafitiwa……………………….........................................21
Jedwali 4.3 Kidato cha mtafitiwa………………………......................................22
Jedwali 4.4 Adui mpende/Anipendaye nampenda, anikataaye namkataa……………24
Jedwali 4.5 Mwenye shoka hakosi kuni/ Penye miti hapana wajenzi…………… .....25
Jedwali 4.6 Nahodha wengi chombo huenda mrama/Panapo wengi hapaharibiki jamb. ..........................................................................................................................27
Jedwali 4.7 Akutendaye ubaya mlipe kwa wema/ Akutendaye mtende…………….28
Jedwali 4.8 Fuata nyuki ule asali/Fuata nyuki ufie mzingani…………………………. ..........................................................................................................................30
Jedwali 4.9 Mavi ya kale hayanuki/Mavi ya kale hayaachi kunuka………………...31
Jedwali 4.10 Ngoja ngoja huumiza matumbo/Mstahimilivu hula mbivu……………… ..........................................................................................................................33
Jedwali 4.11 Adhihakiye kovu hajaona jeraha/Achekaye kilema na kwao kipo…......34
Jedwali 4.14 Jinsia ya mtafitiwa……………………….......................................39
Jedwali 4.15Tajriba kama mwalimu katika shule ya upili…………………………...40
Jedwali 4.16 Tajriba kama mwalimu wa fasihi ya Kiswahili…………………………. ..........................................................................................................................41
Jedwali 4.17 Kidato Anachosomesha Mwalimu……………………….................42
Jedwali 4.18 Tajriba ya mwalimu kama mtahini wa fasihi ya Kiswahili…………… 42
Jedwali 4.19 Utambuzi wa methali kinzani miongoni mwa wanafunzi…………….. 45
Jedwali 4.20 Matumizi ya Methali Kinzani……………………….......................47
Jedwali 4.21 Umuhimu wa Methali Kinzani Katika Fasihi ya Kiswahili…………….. ..........................................................................................................................48
Jedwali 4.22 Changamoto wakati wa kufundisha ukinzani katika methali za Kiswahili. ..........................................................................................................................49

# ORODHA YA MICHORO

Mchoro 4.12 Umuhimu wa ukinzani katika methali za Kiswahili………………… ..35

Chati 4.13 Mielekeo ya wanafunzi kuhusu ukinzani wa methali za Kiswahili… .......37

Mchoro 4.23 Mielekeo wa Walimu Kuhusu Ukinzani wa Methali…………………51

# ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Hojaji kwa Wanafunzi

Kiambatisho I: Hojaji kwa Walimu

Kiambatisho III: Ratiba ya Kazi

Kiambatisho IV: Bajeti

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu kuchunguza mielekeo ya watumiaji lugha ya Kiswahili kuhusiana na ukinzani katika methali. Kwa mfano methali, *Fuata nyuki ule asali* na *Fuata nyuki ufe mzingani*. Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili; nadharia ya mguso na nadharia ya umaanishaji. Katika upande wa ukusanyaji data, utafiti huu ulitumia hojaji kwenda nyanjani na udurusu wa kina kuhusu methali za Kiswahili. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kubaini na kuchanganua mielekeo ya wanafunzi na walimu wa fasihi ya kiswahili kuhusu kuwepo na methali ambazo maana zake zinakinzana. Matokeo yalibaini kwamba idadi kubwa ya watafitiwa ina mwelekeo chanya kuhusiana na suala lililotafitiwa. Baadhi ya sababu zilizochangia watafitiwa kuwa na mwelekeo chanya ni pamoja na maoni kwamba methali hizi zilizo na maana kinyume humsaidia mwanajamii kutafakari kabla ya kuchukua mwelekeo fulani na labda kuepuka matatizo ya baadaye. Mojawapo ya majukumu ya methali ni kushauri. Hivyo basi, ukinzani utakupa nafasi ya kuchagua ushauri unaokufaa binafsi na upi wa kutupilia mbali. Aidha, kila methali huwakilisha hali halisi ya maisha. Maisha yenyewe yamejaa hali kinzani kama vile urafiki/uadui, wema/ubaya, furaha/huzuni na kadhalika. Kwa kuzingatia kauli hii, kila methali huwakilisha hali fulani. Kwa mujibu wa baadhi ya waliotafitiwa, ukinzani huleta mwelekeo hasi. Walitetea kauli hii kwa kusema kuwa methali zinapokinzana huzua utata na hali ya kumchanganya mtumiaji lugha asijue methali gani itamfaa kwani moja inakuongoza huku, nayo nyingine inakutuma kule! Utafiti huu ulibaini kuwa walimu wana changamoto kubwa sana wanapoelezea maana na matumizi ya methali zinazobishana kwa wanafunzi wao. Asilimia mia moja ya walimu wa fasihi waliotafitiwa walitoa changamoto wanazokumbana nazo wanaposomesha suala la ukinzani katika methali za Kiswahili. Ubishi upo katika methali za Kiswahili lakini iwapo kila methali itatumika katika muktadha, hali na kwa hadhira mwafaka suala la ubishi huu halitakuwa changamoto kubwa. Jambo la msingi litakalozingatiwa ni maana (ufaafu) na matumizi ya methali mahususi. Nadharia ya umaanishaji inashikilia kuwa fasihi inapaswa kuwa na maana. Maana itapatikana baada ya kutumia kila methali katika muktadha na mazingira mwafaka, ndiposa mguso au athari ya fasihi ipatikane (ili fasihi iweze kutekeleza jukumu lake katika jamii).

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi.

Sura hii ni kitambulisho cha Tasnifu nzima. Inajumuisha usuli wa mada, suala la utafiti na malengo ya utafiti. Aidha, ni sura inayoshughulikia maswali ya utafiti, umuhimu, upeo na mipaka ya utafiti huu.

## 1.1 Usuli wa Mada

Methali hutumiwa na wazungumzaji, waandishi na katika kazi tofauti tofauti za sanaa kama mapambo ya lugha mahususi. Kila taifa, kila kabila na kila lugha ina methali zake ambazo zinawiana na mazingira yanayotawala watumiaji lugha fulani. Kwa mfano, methali za jamii ya Wakamba zinazunguka mazingira ya eneo la watumiaji lugha hawa.

Kwa kuzingatia methali za Kiswahili tunabaini kwamba ubishi hujitokeza wakati ambapo maana za methali zinapingana au zinatoa maana zilizo kinyume. Kila methali ya Kiswahili huwa na maana yake lakini katika mazingira ambayo methali mbili huwa na maana zilizo kinyume kuhusu suala moja, huu ndio hufahamika kama ukinzani wa methali. *Akutendaye ubaya mlipe kwa wema/ Akutendaye mtende* ni mfano wa methali zilizo na ukinzani ulio wazi. Methali ya kwanza inashawishi wanajamii kutolipiza kisasi huku ya pili ikitoa shinikizo lililo kinyume kabisa; inasisitizia kisasi miongoni mwa wanajamii.

Methali ni semi ambazo hutumiwa na watumiaji lugha kuondoa ukungu katika mawasiliano ambayo yanaonekana kuwa magumu ama yaliyo na usayansi. Neno ‘ukungu’ lina maana ya mawingu meupe ambayo hutanda angani na kusababisha giza. Katika muktadha huu, neno hili lina maana ya ukavu unaoletwa na mawasiliano haswa ya kitaaluma. Methali hutumika katika mawasiliano ili kurahisisha ugumu wa misamiati au mawasiliano ya kitaaluma. Mwandishi Chinua Achebe (1959; 7) ananukuliwa na John (2005) akisisitiza kwamba methali ni mafuta ya mawese ambayo kwayo maneno huliwa. Kwa kuzingatia kauli hii, lugha ya fasihi hutumia methali na fani nyinginezo kama viungo vya kuifanya lugha hii iwe na ladha ya kupendeza miongoni mwa watumiaji wake. Aidha, lazima methali itumike katika muktadha na mazingira mwafaka ili maana ijitokeze. Methali inapotumika pasipohitajika huwa inapoteza maana.

Methali zinaweza kulinganishwa na chakula. Ili chakula kipate ladha ya kupendeza lazima kitiwe viungo tofauti na vichanganywe kwa utaratibu mzuri na wa kupendeza. Vivyo hivyo, methali zinapotumiwa lazima mtumiaji lugha atumie methali mwafaka kwa muktadha mahususi ili kuleta maana katika mawasiliano. Haiwezekani kuchukua methali yoyote tu na 'kuitupa' popote pale katika mawasiliano. Methali hiyo itakosa maana kwani haioani na muktadha mahususi.

Neno ukinzani limefasiliwa na Kamusi ya Kiswahili sanifu (2004) kama hali ya ukaidi na kisawe chake ni upinzani. Upinzani ni hali ya kupinga au kuwa na ubishi kuhusu suala fulani. Hali hii hutokea katika mazingira ya kutokuwepo na mwafaka kuhusu suala au fulani inayojadiliwa au kuzungumziwa. Methali zina sifa hii ya ubishi katika mazingira ambapo maana ya methali moja huwa kinyume na maana ya methali nyingine hivi kwamba mwelekeo unaotolewa na methali moja ni tofauti sana na unaotolewa na methali nyingine.

Methali ni kipera cha utanzu wa semi katika fasihi simulizi. Kulingana na TUKI (2004) methali ni usemi wa kisanii ambao ni wa kimapokeo na jamii huuchukulia kuwa wa kweli na hutumiwa na jamii husika kufumbia au kupigia mfano. Vilevile, methali hubeba maana pana kuliko maneno yanayotumiwa. Kwa mfano, tunaposema kwamba *dawa ya meno ni meno,* neno *meno* limebeba maana zaidi ya kile kipande kigumu na cheupe kilicho kinywani mwa binadamu au mnyama. Neno meno linaweza kumaanisha tabia, mwenendo, hali fulani na hata mwelekeo fulani.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), methali inafasiliwa kama msemo wa kimapokeo na ambao muundo wake ni maalum, unaweza kukumbukika na malengo yake ni kama vile kuadibu, kulaumu, kushauri, na kadhalika. Suala la methali limeshughulikiwa sana katika Paremiolojia. Methali huwa na miundo tofauti tofauti kwa mfano, zipo methali ambazo zimeundwa kwa kutumia maswali ya balagha. Kwa mfano, *kamba haikuwa kamba, itakuwa kambaa?*

Utafiti kuhusu methali umefanywa na watafiti mbalimbali ambao wameshughulikia taaluma hii ambayo ni pana na changamano. Kadiri wachunguzi wanavyozidi kushughulika na kazi yao ya utafiti ndivyo wanavyozidi kufichua maarifa muhimu na

kuyatumia katika nyanja za masomo ya juu ulimwenguni. Hata hivyo, ni wazi kwamba hiki kipera cha methali hakijatafitiwa vya kutosha.

Utafiti huu uliangazia ukinzani katika methali za Kiswahili. Katika uwanja huu mpana wa methali za Kiswahili, ni wazi kwamba zipo methali ambazo hupinga maana ya methali nyingine, hivi kwamba methali moja inatoa ujumbe fulani huku ya pili ikitoa ujumbe unaoonyesha kinyume cha ujumbe uliotangulia. Kwa mfano:

*(i)* *Mavi ya kale hayanuki*
*Mavi ya kale hayaachi kunuka.*

*(ii)* *Ngoja ngoja huumiza matumbo*
*Mstahimilivu hula mbivu.*

Kauli hii ina maana kwamba kila jamii ina methali zake ambazo watumiaji lugha mahususi huzitumia mara kwa mara katika kuwasilisha mawazo tofauti tofauti. Methali zinazohusishwa na jamii fulani huwa amali na sehemu ya utamaduni wa jamii husika. Hata hivyo, kuna methali ambazo hutumika mahali popote duniani. Kwa mujibu wa John (2011) anasema kwamba kuna methali zilizo na uwezo wa kuvuka mipaka na kutumika kwingine ambako lugha yake ni tofauti. Kinachovuka mipaka sio muundo wa methali bali ni maudhui au maana inayotolewa na methali hiyo. Yaani, maneno tofauti hutumika lakini maana huwa sawa. John (2005) ameziita methali hizi methali za kiutandawazi au methali za kimataifa. Kwa mfano, *Wapishi wengi huharibu mchuzi (Too many cooks spoil the broth)* na *Penye njia pana njia (Where there is a will there is also a way)***.**

Lugha yoyote ile hutumia vipashio vyake kuunda fani tofauti za kuirutubisha lugha hiyo. Murithi (2015) anasisitiza kwamba lugha haiwezi kutenganishwa na mwanadamu kwani mwanajamii huyu ndiye muumba wake. Kwa hivyo, lugha hushamiri tu yale yaliyo katika tajriba ya jamii mahususi. Fasihi inayotumiwa katika jamii yoyote inapaswa kusawiri kwa njia ya uwazi kabisa tajriba za wanajamii hawa huku ikileta athari fulani kwa mwanajamii mahususi.

Vilevile, kuna methali nyingine ambazo zina muundo wake wa kutumia tanakali za sauti, uradidi, mchezo wa maneno na kadhalika. Kwa mfano, *Chururu si ndo-ndo-ndo*. Hii ni mbinu ya tanakali za sauti ambayo ni mbinu ya kutumia maneno yanaoiga sauti au namna kitendo kilivyofanyika. Methali pia inaweza kuchukua muundo wa uradidi, kwa mfano, *bandu bandu humaliza gogo,* au hata muundo wa mchezo wa maneno kwa mfano *pema usijapo pema ukipema si pema tena.*

Ukinzani ni ubishi ambao hupatikana katika methali. Methali ni semi ambazo hubeba maana. Ubishi huu hutokea katika mazingira ambapo methali moja inatoa maana fulani huku nyingine ikipinga kinachotigwa na ile ya kwanza. Zipo baadhi ya jozi za methali ambazo mawazo yake hubishana au hutofautiana. Kwa mfano:

*Fuata nyuki ule asali*

*na*

*Fuata nyuki ufie mzingani.*

Huu ni mfano mzuri wa methali zenye ukinzani. Picha ya nyuki/asali na kifo zinajichora akilini mwa mtumiaji wa methali hizi. Methali ya kwanza inamhimiza mwanajamii kufuata nyuki ili kupata asali ambayo kwa kawaida huwa ni tamu sana. Methali ya pili inakinzana na ile ya kwanza kwani inaonya kwamba kufuata nyuki kuna madhara mabaya kwa sababu wadudu hawa wana uwezo wa kasababisha hata kifo cha msakaji asali. Kuna methali nyingi za Kiswahili ambazo zina sifa hii ya ukinzani.

**1.2 Suala la Utafiti**

Waandishi wengi walioshughulikia suala la methali za Kiswahili wameziorodhesha na kufafanua maana na baadhi wakataja matumizi yake. Miongoni mwa waandishi hawa ni Wamitila (2003) na King'ei (1989).Uorodheshaji huu ni muhimu kwani unasaidia katika upatikanaji wa methali za Kiswahili na hivyo kurahisisha tafiti zaidi zinazohusu methali.

Utafiti huu, ulidhamiria kutafutia ufumbuzi na kubaini mielekeo ya watumiaji lugha ya Kiswahili kuhusu suala la ukinzani wa methali za Kiswahili. Hili ni suala ambalo halijashughulikiwa kwa upana. Uchunguzi ulifanywa kwa wanafunzi wa fasihi katika

kiwango cha shule ya upili, kidato cha tatu na cha nne. Vilevile, uchunguzi ulifanywa kwa walimu ambao ndio waelekezi wa somo hili la fasihi kwa wanafunzi waliotafitiwa. Maoni yao yaliauni pakubwa kwani wao wana tajriba na uzoefu wa juu kuhusu methali ikilinganishwa na wanafunzi wao. Kwa mujibu wa Mtesigwa (2013), maana ya methali hutofautiana miongoni mwa watumiaji hata ingawa watumiaji hawa wamewahi kuisikia ikitumiwa.

Methali zina jukumu la kuleta suluhu ya baadhi ya matatizo miongoni mwa watumiaji lugha. Je, methali zinapokinzana huleta suluhisho kama inavyotarajiwa ama huleta utata miongoni mwa watumiaji lugha? Maswali huibuka kuhusu methali itakayofaa kutumiwa wakati huo mahususi ili kutoa suluhisho mwafaka. Kwa mfano:

*Nahodha wengi chombo huenda mrama*

*na*

*Panapo wengi hapaharibiki jambo.*

Katika hali kama hii, upande wowote ule unaweza ukajitetea kwani methali hizi zinakinzana kimaana. Upande mmoja utakashifu ule mwingine kwa kuhusisha watu wengi katika kutatua jambo fulani. Kwa upande mwingine hao wengi watajitetea kwa kuwapingia methali, *panapo wengi hapaharibiki jambo.*

Hali hii ndiyo ilimsukuma mtafiti kufanya utafiti huu lengo likiwa kubaini mielekeo mahususi inayodhihirika kutoka kwa watumiaji lugha, kutokana na ubishi unaoletwa na methali zilizo na maana kinyume. Mielekeo hii inaweza kuwa chanya au hasi kutegemea mtumiaji lugha mmoja hadi yule mwingine.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kutimiza malengo yafuatayo:

1. Kubainisha mielekeo ya wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne kuhusu methali zenye maana kinzani.
2. Kutathmini mielekeo ya wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne kwa kutumia kigezo cha uchanya na uhasi.
3. Kuchanganua mielekeo ya walimu kama waelekezi na watahini wa somo la fasihi ya Kiswahili kuhusu ukinzani katika methali za Kiswahili.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kujibu maswali yafuatayo:

1. Wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne katika kata ya Kitui mjini wanadhihirisha mielekeo ipi kuhusu methali zenye maana kinzani?
2. Mielekeo inayodhihirishwa na wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne katika kata ya Kitui ni chanya au ni hasi?
3. Mielekeo inayodhihirishwa na walimu wa fasihi ya Kiswahili katika kata ya Kitui kuhusu ukinzani wa methali ni chanya au ni hasi?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa wenye manufaa sana kwa wasomi na wapenzi wa fasihi ya Kiswahili. Utafafanua masuala mengi kuhusu methali haswa suala la ukinzani katika methali za Kiswahili ambalo halijashughulikiwa kwa kina katika tafiti zilizotangulia zinazohusiana na methali na ufundishaji wa methali za Kiswahili.

Pili, utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa kwa wanaopanga sera katika taifa hili, haswa sera za elimu. Vitabu ambavyo wanafunzi wanatumia katika masomo ya fasihi vinapaswa kuweka wazi na kufafanua masuala tofauti ya fasihi kwa undani. Methali ni kipera cha semi ambacho wengi wameshughulikia tu katika kuziorodhesha, kutoa maana na matumizi yake na wengine kutaja miundo ya methali. Kazi hii imechangia mno kwa kushughulikia ukinzani wa methali na hata athari za ukinzani huu kwa watumiaji lugha.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Katika utafiti huu, watafiti walilenga kushughulikia methali za Kiswahili na ambazo ni kinzani peke yake. Japo kuna methali nyingi za Kiswahili ambazo zimeorodheshwa na wasomi tofauti, utafiti huu haukuzishughulikia zote, ila tu zile ambazo zina ujumbe au maana kinzani. Utafiti huu ulijikita katika jozi ishirini za methali zinazokinzana peke yake. Kuna methali nyingi zinazokinzana lakini mtafiti alijifunga katika idadi hii ya methali zinazotoa ujumbe ulio na ukinzani. Jozi hizi zinatosha kuwa sampuli wakilishi ya methali zote za Kiswahili zinazotoa maana zenye ukinzani. Watafiti walichambua methali hizi na kuonyesha kwa uwazi namna ukinzani unavyojitokeza katika kila jozi.

Katika ukusanyaji wa data, watafiti walipata data kutoka kwa wanafunzi wa fasihi (Kidato cha tatu na cha nne) kutoka kwa baadhi ya shule za upili katika kata ya Kitui Township, kaunti ya Kitui na kutoka kwa walimu wa fasihi ya Kiswahili. Ufinyu wa muda wa kufanya utafiti huu uliwalazimu watafiti kuchagua eneo hili ambalo umbali wa sampuli iliyotafitiwa hukuwa changamoto kubwa kwa watafiti. Tuliandaa hojaji za wanafunzi wa kidato cha tatu na nne na za walimu wa fasihi ya Kiswahili ili kupata data waliyonayo na inayohusiana na suala hili la utafiti.

# SURA YA PILI

# UDURUSU WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusiana na suala la methali kwa jumla. Wasomi wengi wa fasihi ya Kiswahili wamelitafitia suala hili la methali kwa upana, ikiwemo kuziorodhesha, kuonyesha umuhimu wake na hata kutaja matumizi ya methali hizi za Kiswahili. Katika sura hii, utafiti huu ulijikita katika maandishi yanayohusiana na ukinzani katika methali za Kiswahili. Ni katika sura hii ya pili ambapo mtafiti ametaja na kufafanua nadharia ambazo ziliuongoza na kufanikisha utafiti huu.

## 2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kuna mengi yaliyoandikwa kuhusu methali kama utanzu wa fasihi simulizi lakini suala la ukinzani katika methali halijashughulikiwa vya kutosha haswa katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia kwa kina athari zinazoletwa na ukinzani wa methali za Kiswahili kwa watumiaji wa lugha hii. Kwa mujibu wa Yankah (1994), wanadamu wana uelewa mkubwa wa kuwepo kwa methali kinzani katika lugha. Anatoa mifano ya jozi ya methali ambayo ni kinzani katika lugha ya Kiingereza;

"*Absence makes the heart go fonder*" ni methali ambayo ilichapishwa mara ya kwanza katika kitabu cha mashairi cha Francis Davison's *Poetical Rhapsody* mwaka wa 1602 inayokinzana na methali *"Out of sight out of mind"* ambayo inaoana kimaana na methali ya Kiswahili, *'Asiyekuwepo na lake halipo'*. Hata hivyo, anasisitiza kuwa ukinzani huu haupaswi kuwa jambo la ajabu sana kwani methali ni semi za hekima ambazo hutumiwa tu katika mazingira mahususi na jamii au watu fulani. Kinachotiliwa mkazo na kauli hii ni kwamba methali zikitumiwa katika muktadha na matumizi yanayofaa, basi ukinzani huwa haupatikani. Methali hupata maana yake ikitumika katika muktadha unaofaa.

Kawaida, methali hujengwa na mazingira kwani misamiati inayopatikana katika methali inaoana na mazingira fulani. Hii ndio sababu tutashuhudia baadhi ya methali ambazo zinapatikana na kutumiwa tu na wanajamii mahususi. Fasili nyingi za fasihi huwa zimeegemea kuielezea katika uhusiano wake na jamii. Fasili hizi zinadhihirisha

wazi kwamba fasihi ni taasisi ya jamii na uhusiano wake na jamii hauwezi kupuuzwa. Escarpit (1974; 4) anatoa maoni yanayokubaliana na haya ya Escarpit anaposema kwamba lazima fasihi ichukuliwe kama iliyo na uhusiano usiotatanika na uhusiano wa kijamii. Fasihi huwakilisha maisha na maisha haya kwa upana huonyesha uhalisia wa jamii.

Methali bado zina maana. Nzookwa (2002) anasema kwamba methali fulani hutolewa kama mukhtasari wa uzoefu alionao mtu katika jambo fulani au jamii mahususi. Jamii husikika ikitumia methali kila uchao bila kuzingatia iwapo ni ya zamani au ya sasa. Methali mpya huzidi kuundwa kulingana na jamii inavyozidi kukabiliana na matukio tofauti katika maisha yao. Methali hueleza mawazo mazito au fikra kutokana na uzoefu wa wanajamii. Iwapo binadamu fulani hana uzoefu wa kutosha katika shughuli fulani, itakuwa vigumu kupata methali ya kutumia kama mukhtasari wa kauli aliyotaka kuitoa. Methali inapaswa kutoa ujumbe fulani na lazima mtu huyu atoe methali inayofaa muktadha husika.

Mieder na Litovkina (1999) na Mieder (2007) wanasema kwamba methali huzaliwa kila siku. Kulingana nao, methali huwa muundo wa mada na maelezo ya mada hiyo. Methali huwa na sehemu mbili ambapo sehemu ya kwanza hutoa hoja huku sehemu ya pili ikikamilisha au hata kukanusha sehemu hiyo ya kwanza. Kwa mfano, *'asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu'*.

Kuhusiana na suala la ukinzani katika methali, waandishi hawa wanasema kwamba katika siku za hivi karibuni watumiaji lugha wanazipinda methali za Kiswahili ili kuleta hali dhihaka lakini iliyo na ukweli. Wanatoa mfano wa mwandishi Zakaria Mochiwa (1988) ambaye alipinda methali isemayo *'mvumilivu hula mbivu'* ikawa *'mvumilivu hula mbovu'.* Katika uwanda mkubwa wa methali kuna mazingira ya methali kongwe, methali pindwa na methali ibukizi. Hizi ni njia tofauti za kufikisha ujumbe ulio ndani ya methali.

Methali huundwa kwa sababu kadhaa na kwa njia tofauti. Nzookwa (ametajwa), anasema kwamba zipo methali ambazo hutokea kama kauli ya kawaida na hatimaye kupandishwa hadhi ya methali. Ni wazi kwamba methali hutumiwa mara kwa mara kutegemea muktadha fulani. Zipo methali za Kiswahili ambazo zinatofautiana kwa

namna fulani lakini huonyesha uhusiano wa matumizi yake. Kwa mfano, *huwezi kumwashia jirani taa na hali kwako kuna giza*. Methali hii inahusiana kimaana na ile inasema kwamba, *usiache kwako kumezimika ukaenda kuwasha kwa jirani.* Vilevile, kuna methali nyingi za Kiswahili ambazo zinatoa ujumbe kinyume. Hili ndilo suala ambalo utafiti huu utajikita kwalo.

Katika karne ya kwanza, mwandishi wa Kirumi aitwaye Lucretius alitoa methali ambayo katika mwaka wa 1604 ilifanywa kuwa methali katika lugha ya Kiingereza; *'One man's meat is another man's poison'*. Katika lugha ya Kiswahili, ipo methali inayooana kimaana na hii ya Lucretius isemayo, *'Mkuki kwa nguruwe mtamu, kwa binadamu mchungu*.' Methali hii ina maana kwamba unachokipenda huenda kikawa chukizo kwa mtu mwingine. Methali hizi mbili zinapatikana miongoni mwa watumiaji lugha tofauti lakini maana na matumizi yake yanasawiana. Katika maisha ya kawaida, watu huwa na hisia tofauti kuhusu jambo au hali fulani. Ujumbe huu hutumiwa kumsuta mtu ambaye hupenda kuwahujumu wengine lakini wakati wake wa kuhujumiwa ukifika atalalamika kwamba anaonewa.

Hata hivyo katika mwaka wa 1546, John Heywood alikuwa keshatoa msemo unaokinzana na ule wa Lucretius (1602) usemao, *'What good for the goose is good for the gander'*, ikiwa na maana kwamba kilicho kizuri kwako hata kwa mwingine ni vivyo hivyo. Methali hii ina maana kwamba kilicho chema kwa mtu mmoja, bila shaka kitakuwa chema kwa binadamu mwengine pia.

Kwa kufafanua methali hizo mbili nilizotaja hapo juu; *Absence makes the heart go fonder* inatumiwa sana na watu wanaopendana na ina maana kwamba kadri mmoja anavyokuwa mbali na mwenzake, mapenzi nayo yanazidi kunoga. Methali hii ina maana kinyume na inayosema kwamba 'kisicho machoni na moyoni hakipo pia'.

Methali *'Out of sight out of mind'* inakinzana na methali *'absence makes heart go fender'*, kwamba kisicho machoni na moyoni hakipo pia na bila shaka kitasahaulika. Kwa mfano, mtu akienda kuishi mbali na mpenziwe, mara nyingi mapenzi kati yao hupungua na hata wengine huweza kufikia kiwango cha kutengana. Utengano huu husabishwa na umbali kati ya hawa wapendanao. Ukinzani katika methali hizi mbili utapatikana iwapo kwa mfano, aliyezoeana na mpenziwe ama rafikiye wa karibu

watatenganishwa. Katika hali hii ya upweke methali *'absence makes the heart go fonder'* huenda itakosa maana mbele ya upeo wa mtu huyu. Je, wahenga katika hawakusema kwamba *'fimbo ya mbali haiui nyoka'?*

Yankah (1994) anazidi kufafanua suala hili la ukinzani wa methali kwa kusema kwamba, iwapo mtu atachukulia miwani kama jambo au hali halisi katika jamii fulani, basi ukinzani hautakosekana katika methali zinazopatikana katika jamii hiyo. Hivyo basi anatoa maoni kwamba iwapo methali itatumiwa katika na kulingana na mazingira mahususi na yanayofaa, basi ukinzani katika methali hautapatikana [utafsiri]. Kawaida, methali hujengwa na mazingira kwani misamiati inayopatikana katika methali inaoana na mazingira fulani. Hii ndio sababu tutashuhudia baadhi ya methali ambazo zinapatikana na kutumiwa tu na wanajamii mahususi. Kwa mfano, *"mgaagaa na upwa hali wali mkavu"* ni methali ambayo iwapo tutazingatia maana ya nje, watakayoielewa vyema na haraka ni wale tu ambao wanapatikana katika maeneo ambayo misamiati kama vile upwa na wali inatumika.

**2.3 Fasili ya Methali**

Kimsingi, methali ni semi. Hata hivyo, semi hizi zina sifa ambazo huzitofautisha na semi zingine za fasihi. Sifa hizi bainifu ni zile ambazo zinahusiana na dhima yake kama kitambulisho na falsafa ya jamii inayohusika na usemi wenye ulinganifu na usemi wa maisha ya kila siku. Wataalamu mbalimbali waliozitafitia methali kwa kina wamefanikiwa kutaja na kufafanua baadhi ya sifa hizi mahususi. Ngole na Honero (2004: viii) wamenukuliwa na Mtesingwa (2013) wakieleza kwamba:

> Methali ni aina moja ya usemi mzito na ambao unakusudiwa kusema jambo maalumu lakini kwa namna ya fumbo. Usemi huu mzito mara nyingi hukusudiwa kumuonya, kumuongoza na kumuadilisha mwanadamu…

Kamusi zimeelezea maana ya methali kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya methali. Kamusi sanifu ya Kiswahili Sanifu (2004; 240) inaelezea methali kama ni:

> Usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano au huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.

Kutokana na maelezo haya, inabainika kwamba methali hutumia maneno ya kifalsafa yenye maana nzito na yanayoleta mguso kwa jamii. Vilevile, methali hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

### 2.4 Uainishaji wa Methali

Kwa mujibu wa Wamitila (2012), *uainishaji* ni upanguaji wa makundi kwa kuzingatia sifa fulani zinazofanana na zinazoweza kuwa mbinu za lugha zilizotumiwa au hata sifa fulani za kimuundo. Katika taaluma ya Paremiolojia, kuna vigezo ambavyo hutumiwa kuainisha au kuzipanga methali katika makundi yanayohusiana. Vigezo hivi ni kama vile: kigezo cha kimaana, kiuamilifu, kimuundo, kialfabeti na kimuktadha.

#### 2.4.1 Kigezo cha Kimaana

Kinachochunguzwa hapa ni maana za methali. Msingi wa uainishaji wa methali kwa kuzingatia kigezo hiki ni kuwasilisha maana mbalimbali. Hili linaweza kufikiwa kwa kuangalia tamathali zilizotumiwa. Tunaweza kupata aina kama vile:

*(i)* *Methali za chuku*

a) Usipoziba ufa, utajenga ukuta
b) Mzigo wa mwenzio, ni kanda la usufi

*(i)* *Methali za kisitiari*

a) Majuto ni mjukuu, mwisho huja kinyume
b) Debe tupu haliachi kuvuma

*(ii)* *Methali za kikweli- kinzani*

(a) Kupotea njia ndiko kujua njia
(b) Simba mwenda pole ndiye mla nyama

### 2.4.2 Kigezo cha Kiuamilifu

Uamilifu ni utenda-kazi wa malengo au kazi fulani. Kinachotiliwa maanani hapa ni kazi inayotekelezwa na methali fulani. Hii ni ndiyo sababu mara kwa mara huwa tunasikia watu wakisema kuwa methali huweza kutumiwa kuonya, kuadibu, kuunganisha jamii pamoja, kushauri, kukejeli na kadhalika. Kwa mfano:

*Jukumu la kushauri*

a) Pole pole ndiyo mwendo
b) Asiyefunzwa na mama hufunzwa na ulimwengu

*Jukumu la kuonya*

a). Usipoziba ufa utajenga ukuta

*Jukumu la kuunganisha jamii pamoja*

a). Kidole kimoja hakivunji chawa
b). Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu

### 2.4.3 Kigezo cha Kimuundo/Kimtindo

Katika kigezo hiki, methali huainishwa kwa kuzingatia sifa za kimuundo katika methali fulani. Sifa hizi ni kama vile: takriri za irabu au konsonanti, tanakali za sauti, mchezo wa maneno, n.k.

(i). *Mchezo wa maneno*

a). Pema usijapo pema;ukipema si pema tena
b). Ukiambwa jambwe usijeamba kumbe

(ii) *Tanakali za sauti*

a) Maskini akipata matako, *hulia mbwata!*
b) Chururu si *ndo- ndo- ndo!*

(iii)*Uradidi*

a) *Hayawi hayawi* huwa
b) *Bandu bandu* humaliza gogo

### 2.4.4 Kigezo cha Kialfabeti

Vitabu mbalimbali ambavyo vimekusanya methali za jamii tofauti hutumia kigezo hiki cha kialfabeti. Methali huorodheshwa kwa kuzingatia herufi zake za kwanza bila kuzingatia muundo wala dhamira ya methali husika.

### 2.4.5 Kigezo cha Kimuktadha

Jambo muhimu la kuzingatia katika uainishaji huu ni kuangalia dhamira ya methali husika. Katika kufuata utaratibu huu, mchunguzi anapaswa kubainisha dhamira ya methali anayotumia na kuilinganisha na nyingine. Hivyo basi, methali zilizo na dhamira sawa zinaweza kuwekwa katika kundi moja. Kwa mfano kuna methali zilizo na dhamira ya ndoa, ugomvi, malezi, dini, kifo, ugomvi, n.k. Hata hivyo kuna methali zilizo na dhamira zaidi ya moja, yaani, zinaweza kutumiwa katika hali nyingi na tofauti.

## 2.5 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umejengeka kinadharia katika nadharia mbili; ya *mguso* na ya *umaanishaji*. Nadharia ya mguso inasisitiza kwamba lazima fasihi iwe inamlenga mtu au watu fulani kwa njia moja ama nyingine ili kuwafanya waifikirie fasihi hiyo kwa undani wa aina yake. Kwa upande wa pili, nadharia ya umaanishaji nayo husisitiza maana katika mawasiliano ambapo lazima wanaohusika waelewe maana inayojitokeza katika fasihi husika.

### 2.5.1 Nadharia ya mguso

Nadharia ya mguso inafafanuliwa kwa kina na Ntarangwi (2004:14) ambapo anaihusisha nadharia hii na jamii. Anasema kwamba, kila kazi ya fasihi huwa inamlenga mtu au kundi la watu fulani kwa namna kwamba lazima itoe mguso fulani kwa hadhira hiyo. Hadhira basi itafikiria zaidi na hata kujiuliza maswali kuhusu fasihi hiyo na basi kupata funzo fulani kutokana na fasihi hiyo. Ntarangwi anatoa maoni yanayosawiana na maoni ya Vasquez A.S (1973; 113) ambaye anasema kwamba:

> …kazi ya sanaa huathiri watu na huchangia katika kuhimiza au kupuuza dhana zao, maazimio yao na hata maadili yao-ina msukumo wa kijamii ambao huathiri watu kwa nguvu zake za kihisia na kiitikadi. Ama kwa hakika, hakuna anayebaki vile vile baada ya kuguswa na kazi halisi ya sanaa. [Tafsiri]

Kwa mujibu wa Vasquez A.S basi, lazima fasihi iwe na athari fulani katika maisha ya binadamu husika na mguso huu utampa msukumo fulani ambao utamwelekeza katika kuathirika kihisia au hata kitabia. Anasisitiza kwamba unapoguswa na fasihi huwezi ukabaki kama ulivyokuwa hapo awali. Kwa kutolea hoja hii mfano, unapokuwa katika

hali ya wasiwasi kwamba hufikii malengo yako maishani kisha uambiwe methali kwamba, *"Kupotea njia ndiko kujua njia."* Mwanajamii anahimizwa kwamba asichoke kujaribu zaidi na zaidi kwani siku moja atafanikiwa. Hivi ni kumaanisha kwamba itakugusa kihisia na kukuhimiza usonge mbele.

Kwa ujumla, nadharia hii inashikilia kwamba kazi ya fasihi lazima iwe inalenga mtu au kundi fulani la watu. Methali kama utanzu wa fasihi zinapaswa kuleta mguso fulani kwa watumiaji lugha. Fasihi ina msukumo wa kijamii unaochangia katika kuathiri jamii husikika kitabia, kimsimamo na kiitikadi. Kauli hii inasisitiza kwamba fasihi huleta badiliko fulani katika maisha ya mwanajamii. Wellek na Warren (1949:102) wanashuhudia kuwa watu wamewahi kubadilisha mienendo yao katika maisha kwa kuathiriwa na wahusika wa kubuni katika fasihi.

Katika utafiti huu, maoni ya wanafunzi na walimu wa fasihi yalisaidia katika kutathmini mguso unaoletwa na methali kinzani. Kwa hakika mielekeo yao kuhusu suala hili linalotafitiwa, ni mojawapo wa mguso unaoletwa na ukinzani katika methali. Athari anayoipata mwanajamii mahususi kutokana na ukinzani wa methali iliongoza katika kutosheleza malengo ya utafiti huu. Watafiti waliongozwa na maoni ya kila mtafitiwa katika kubainisha mwelekeo wao kuhusu ukinzani wa methali na baadaye kubaini iwapo mwelekeo huu ni chanya au ni mwelekeo hasi. Nadharia hii inasisitizia kuwepo kwa mguso fulani kutokana na kazi ya fasihi. Mhimili huu uliongoza utafiti huu katika kubaini mielekeo ya wanafunzi kutokana na mguso au athari wanayopata wanapokabiliana na suala la ukinzani wa methali.

Ijapokuwa nadharia hii ya mguso ina changamoto ya kutathmini kiwango cha mguso, katika utafiti huu nina matumaini kwamba data iliyokusanywa ilisaidia katika kukabiliana na changamoto hii.

### 2.5.2 Nadharia ya umaanishaji

Umaanishaji ni neno ambalo msingi wake unahusiana na dhana ya 'maana'. Nadharia hii ya umaanishaji iliasisiwa na Grice (1975). Mhimili wake wa msingi kabisa ni kwamba katika fasihi, mambo huwa hayasemwi waziwazi. Ili kuelewa kinachosemwa lazima pawepo na umaanishaji katika maana.

Wasemaji huweza kumaanisha mambo yanayozidi wanachokisema. Kauli hii ina maana kwamba fasihi hutumia lugha, ambapo neno moja linaweza kuwa na maana zaidi ya ile ya msingi. Hivyo basi, lazima msikilizaji aelewe na kuchanganua kisemwacho ili mawasiliano yawepo. Methali ni mojawapo ya fasihi ambayo huwa na aina mbili za maana, maana ya wazi na maana fiche. Kwa mfano, '*Usiache mbachao kwa msala upitao'*. Kwa kuangalia maana ya juu, '*Mbachao*' ni kifaa duni kinachotumiwa kufanyia ibada au mkeka au jamvi kuukuu? '*Msala'* nao ni sehemu ya kusalia lakini sio duni kama ilivyo mbachao. Maana fiche ni kwamba, usiache marafiki au hata mambo yako ya zamani kwa sababu kuna marafiki wapya ambao wamejitokeza. Marafiki hawa wapya wanaweza wakakutenga mara tu unapopatwa na changamoto fulani, lakini wale wa zamani watabakia upande wako.

Nadharia hii inashikilia kuwa maana hutokana na ushirikiano baina ya msikilizaji na msemaji. Hoja hii ina maana kwamba lazima makundi haya mawili yaelewe muktadha na mazingira ya fasihi husika. Hivyo basi, nadharia hii inatusaidia kufahamu kwamba jambo la msingi la chochote kisemwacho ni maana. Iwapo mtu fulani hataelewa hata maana ya msingi ya maneno yanayotumiwa katika methali za Kiswahili, huenda asielewe maana inayoletwa na methali hiyo. Pili, hataweza kuona ukinzani katika methali alizotajiwa wala kuzihusisha methali hizi na mazingira yaliyomo.

Nadharia hii inasisitiza namna ambavyo maana ya maneno katika methali yalivyo muhimu hata kuliko maneno yenyewe. Kwa mfano, iwapo mtu akikupigia methali; "*usitukane wakunga, uzazi ungalipo*", hii ni methali ambayo maana yake ya ndani ni muhimu sana kuliko maneno yenyewe. Ni methali ambayo inaweza ikatumiwa kwa mtoto {ambaye hana haja na mkunga}, wanaume au hata kina mama ambao wana uelewa mkubwa sana wa mkunga na umuhimu wake katika jamii. Neno mkunga ni neno ambalo linabeba maana nyingi. Kwa hivyo anayepigiwa methali hii lazima auhusishe ukunga huu na maisha au mazingira yake halisi na sio tu katika mazingira ya uzazi. Maana ya ndani ya neno mkunga, inaweza kuwa mtu yeyote katika maisha yako ambaye ana uwezo wa kukuauni kwa njia moja au nyingine.

# SURA YA TATU
# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua kwa undani mchakato mzima uliotumiwa katika kupata data inayohusiana na utafiti huu. Masuala yanayojadiliwa katika sura ya tatu ni mtindo wa utafiti, namna sampuli ilivyoteuliwa, ukusanyaji wa data nyanjani, uchanganuzi wa data iliyokusanywa kisha uwasilishaji wa data hiyo.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Kwa mujibu wa Orodho (2003), muundo wa utafiti ni mikakati ambayo hutumiwa kuzua au kujibu maswali ya utafiti. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ambapo mbinu ya kuuliza maswali katika ukusanyaji wa data ilitumika. Maswali haya yalijumuishwa katika hojaji. Aidha utafiti huu ulifanywa nyanjani na maktabani.Aidha, utafiti huu uliegemea katika takwimu kutokana na data zake kuwa katika mfumo wa kimaelezo. Maswali yaliyoundwa kudhibitisha malengo na maswali ya utafiti yalikuwa maswali wazi. Isitoshe, maswali funge yalitumika hasa sehemu ya kwanza inayohusu habari za kibinafsi.

## 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Grace (2013) anamnukuu Kothari (2004) na kusisitiza kwamba kuna aina tofauti za sampuli. Aidha, utafiti huu ulijikita katika aina tatu za usampulishaji ambapo watafitiwa waliteuliwa kwa kuzingatia sifa maalumu ili kuwaweka katika makundi mahususi ili kurahisisha ukusanyaji wa data nyanjani.

Katika utafiti huu, sampuli ilihusisha uteuzi wa eneo la utafiti, shule na wanafunzi. Utafiti ulifanywa katika shule za upili za kutoka kata ya Kitui mjini. Eneo hili limeteuliwa kwa kutumia sampuli kutegemea fursa kwa kuzingatia kuwa ni eneo ambalo lina sampuli inayohitajika katika utafiti na pia kwa kuzingatia kigezo cha ufinyu wa muda alionao mtafiti kukamilisha utafiti wake.

Utafiti ulihusisha shule nane kati ya shule kumi na tatu za upili katika kata hii. Shule hizi zilizoshirikishwa ziliteuliwa kinasibu. Wanafunzi walioteuliwa ni wa vidato vya tatu na nne ikizingatiwa kwamba wamezitumia methali kwa muda wa kutosha na

wametangamana na fasihi na kuisoma kwa undani. Jumla ya wanafunzi kumi waliteuliwa kimakusudi kutoka kila shule. Ili kumpa kila mwanafunzi nafasi sawa ya kuteuliwa kushiriki katika zoezi hili, njia ya sampuli nasibu ilitumiwa. Wanafunzi hawa walipokwishateuliwa, mtafiti alikutana nao na kuwaongoza katika kujibu maswali ya hojaji.

Aidha, walimu wanaofunza soma la fasihi katika kidato cha tatu na cha nne waliteuliwa kimakusudi haswa katika shule ambazo zina walimu wa fasihi zaidi ya mmoja. Sababu za kuteua walimu kama watafitiwa katika utafiti huu ni kwamba; kwanza, ni watumiaji wa methali za Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku. Pili, ni waelekezi wa somo la fasihi hivyo basi wanawaelewa wanafunzi wao kwa namna wanavyotumia methali za Kiswahili katika maandishi na mawasiliano. Maoni yao yalikuwa ya msaada mkubwa sana katika utafiti huu. Katika shule ambazo zina walimu wawili wa fasihi, walimu hawa wote walishiriki katika kujaza hojaji za utafiti huu. Jedwali 3.1 linaonyesha namna wanafunzi na walimu walivyoteuliwa kutoka shule tofauti na idadi yake.

**Jedwali 3.1: Orodha ya Shule ambapo Uchunguzi Ulifanywa**

| Jina la shule | Idadi ya wanafunzi | Idadi ya walimu |
|---|---|---|
| Shule ya wavulana ya Kitui | 10 | 3 |
| Shule ya wasichana ya St. Ursula | 10 | 3 |
| Shule ya mseto ya Kwa- Ngindu | 10 | 1 |
| Shule ya mseto ya Muslim | 10 | 2 |
| Shule ya wavulana ya St. Charles Lwanga | 10 | 3 |
| Shule ya mseto ya Katyethoka | 10 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kaveta St. Stephen | 10 | 1 |
| Shule ya mseto ya Mbusyani | 10 | 1 |
| **Jumla** | **80** | **15** |

### 3.4 Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alitumia mbinu mbili za ukusanyaji wa data nazo ni utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani.

#### 3.4.1 Hojaji

Hojaji ni kifaa cha utafiti kilichotumiwa kufanikisha utafiti wa nyanjani. Mtafiti alitumia hojaji aina mbili ambapo moja iliwalenga wanafunzi na nyingine ilikuwa ya walimu wa fasihi ya Kiswahili.

Maswali katika hojaji ya walimu yalisaidia kutathmini zaidi uelewa wa wanafunzi kuhusu methali kinzani, iwapo katika mawasiliano na utunzi wao wa insha wanatumia methali ipasavyo na kubaini iwapo wanafunzi hutatizika kuchagua methali kulingana na muktadha katika maongezi na katika utunzi.

#### 3.4.2 Mbinu ya maktabani

Mtafiti alilazimika kutumia mbinu ya maktabani ili kusoma na kujifahamisha na methali zilizoorodheshwa na wasomi tofauti kisha kuteua zile ambazo zina ubishi wa maana. Vilevile, mbinu hii ilijikita na udurusu wa kina wa tafiti za awali zinazohusiana na ukinzani katika methali za Kiswahili.

### 3.5 Uchanganuzi wa Data

Baada ya kukusanya data, mtafiti alikuwa na jukumu la kuichanganua data aliyoikusanya nyanjani. Mwelekeo wa kuchambua data kitakwimu na kimaelezo ulifuatwa. Baada ya kuchanganua data iliyokusanywa mtafiti aliwasilisha matokeo ya utafiti wake.

Mchakato uliofuatwa ni wa kuchanganua maoni ya watafitiwa kuhusu ukinzani wa methali katika hojaji A na hojaji B kwa kutumia programu ya SPSS. Data ya walimu na wanafunzi ilichanganuliwa kwa njia tofauti. Maoni ya watafitiwa hawa wote yalisaidia mtafiti katika kubaini mwelekeo na msimamo wa watafitiwa kuhusu suala la ukinzani wa methali katika lugha ya Kiswahili. Methali zilizoorodheshwa zilichambuliwa kimaelezo ili kuafikiana na malengo ya utafiti.

### 3.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Kwa kuzingatia maoni ya Mugenda na Mugenda (2012), uwasilishaji wa matokeo unahusisha kuelewa, kueleza na kufasili data iliyochanganuliwa. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na kitakwimu. Mchoro, chati na majedwali yalitumiwa kuonyesha tarakimu kamili ya idadi ya wanafunzi na walimu wenye mtazamo hasi au chanya. Takwimu hizi zilitumika kama msingi wa kujibia maswali ya utafiti na hatimaye katika kutoa mapendekezo.

Ripoti ya utafiti huu imepangwa katika sura tano. Sura ya kwanza inahusisha masuala ya kimsingi ya utafiti huu, yakiwemo usuli wa mada, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti na upeo na mipaka. Sura ya pili imehusisha kubukua yaliyoandikwa na yale yanahusiana na utafiti huu. Nadharia zinazoongoza utafiti zipo katika sura hii. Sura ya tatu na ya nne imehusika na masuala ya ukusanyaji data, namna ya kuikusanya na namna ya kuichanganua. Sura ya nne imeshughulikia matokeo ya utafiti huu kutoka nyanjani na maktabani. Sura ya mwisho imehusisha mukhtasari wa kazi, hitimisho na mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

## 4.0. Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uchanganuzi na ufasili wa data iliyokusanywa nyanjani kutoka kwa wanafunzi na walimu wa fasihi ya Kiswahili kuhusu suala la ukinzani wa methali za Kiswahili ili kupata mielekeo yao kuhusiana na hili. Watafitiwa 95 walihusika katika kujibu maswali ya hojaji zilizotayarishwa na mtafiti. Matokeo ya utafiti huu yalichanganuliwa na kufasiliwa kwa kutumia SPSS. Jedwali 4.1 linaelezea kitakwimu namna hojaji hizi zilivyogawanywa, kujazwa na kurejeshwa kutegemea na aina ya watafitiwa:

## 4.1. Hojaji zilizojazwa na kurudishwa

**Jedwali 4.1: Hojaji zilizojazwa na kurudishwa**

| Watafitiwa | Hojaji zilizojazwa kikamilifu | Hojaji ambazo hazikujazwa kikamilifu | Jumla | Asilimia ya zilizojazwa kikamilifu |
|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi Kidato 3 na 4 | 73 | 7 | 80 | 91.25 |
| Walimu | 15 | 0 | 15 | 100 |
| **Jumla** | **88** | **7** | **95** | **92.63** |

Hojaji zote tisini na tano zilijazwa na kurudishwa kwa mtafiti. Hata hivyo, sio hojaji zote zilizojazwa kikamilifu. Zile ambazo hazikujazwa kikamilifu hazikutumiwa katika uchanganuzi wa data kwa sababu hazikutoa habari iliyotakikana na mtafiti ili kufanikisha utafiti huu. Watafitiwa katika kidato cha tatu na cha nne walifanikisha utafiti huu kwa kujaza hojaji sabini na tatu, kikamilifu ambazo zilichanganuliwa. Hojaji saba kutoka kwa wanafunzi zilikuwa zimejazwa sehemu ya kwanza pekee; watafiti walizitupilia mbali. Hojaji zote kumi na tano za walimu zilijazwa kikamilifu na kwa ustadi na zikachanganuliwa.

Jumla ya hojaji zilizopeanwa kwa watafitiwa ni tisini na tano na zilizojazwa kikamilifu ni hojaji themanini na saba zikichukua asilimia 92.6. Asilimia hii ilitosha kupata data iliyohitajika kufanikisha utafiti huu.

## 4.2 Utangulizi wa Habari za Msingi za Wanafunzi

### 4.2.1 Jinsia ya watafitiwa

Katika sehemu hii, watafiti walidhamiria kufahamu jinsia ya watafitiwa. Walioshiriki katika utafiti huu waliulizwa kutaja jinsia yao. Katika jamii ya sasa, usawa wa kijinsia ni jambo muhimu na ambalo huzingatiwa katika kila shughuli ya maisha ya mwanadamu iwe masomo, kazi na hata katika masuala yanayohusiana na dini. Kutokana na tetesi hii mtafiti hakuwa na budi kujifahamisha na jinsia ya watafitiwa wake.  Matokeo ya sehemu hii yako katika jedwali 4.2:

**Jedwali 4.2 Jinsia ya mtafitiwa**

| Jinsia | Idadi | Asilimia | Asilimia halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Kiume | 39 | 53.4 | 53.4 | 53.4 |
| Kike | 34 | 46.6 | 46.6 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Kutokana na matokeo katika jedwali 4.2 kati ya wanafunzi 73 waliohusika katika kujaza hojaji za utafiti huu, 39 walikuwa wa jinsia ya kiume huku 34 wakiwa wa jinsia ya kike. Tofauti hii sio pana ikiwa na maana kwamba hakuna jinsia iliyopendelewa.

Idadi kubwa ya shule zilizohusika katika utafiti huu ni za mseto. Hivyo basi, mtafiti alilazimika kubaini jinsia ya kila mtafitiwa ili kuhakikisha kwamba data anayoikusanya haijaegemea upande wa jinsia moja. Maoni yaliyotokana na utafiti huu yamejengeka katika jinsia ya kike na ya kiume. Ingawa idadi ya wanafunzi wa kiume ilikuwa juu, matokeo ya sehemu hii yanabainisha wazi kwamba hakuna jinsia haijawakilishwa ipasavyo kushiriki katika utafiti huu.

### 4.2.2 Kidato cha Mtafitiwa

Watafiti walilenga kujua kidato cha kila mwanafunzi aliyeshiriki katika utafiti huu. Mtafitiwa alitarajiwa kuweka alama ya vema ndani ya kisanduku kilicho karibu na kidato chake. Matokeo ya sehemu hii yanaonyeshwa na jedwali 4.3 lifuatalo:

**Jedwali 4.3: Kidato cha mtafitiwa**

| Kidato | Idadi | Asilimia | Asilimia halisi | Asilimia jumuisha |
|---|---|---|---|---|
| Kidato 3 | 35 | 47.9 | 47.9 | 47.9 |
| Kidato 4 | 38 | 52.1 | 52.1 | 100.0 |
| **Jumla** | **73** | **100.0** | **100.0** | |

Kati ya wanafunzi waliotafitiwa, watafitiwa thelathini na watano ambao ni asilimia 47.9 walikuwa wa kidato cha tatu na wanafunzi thelathini na nane ambao ni asilimia 52.1 walikuwa wa kidato cha nne.

Kigezo cha kidato cha mwanafunzi mahususi ni muhimu sana kwani kwa kuzingatia silabasi ya kiwango cha shule ya upili, wanafunzi wa kidato cha nne wametangamana sana na fasihi ya Kiswahili ikilinganishwa na wale wa kidato cha tatu. Hii ina maana kwamba mawazo ya wanafunzi wa kidato cha tatu hayajapevuka kama ya wenzao wa kidato cha nne.

## 4.3 Ukinzani Unavyojitokeza ndani ya Baadhi ya Jozi za Methali

### 4.3.1 Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo/ Sikio la kufa halisikii dawa

*Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo* ni methali ambayo msingi na maana yake inajikita sana katika msingi wa kifamilia. Baba na mama ndio uhusika kabla na baada ya kuzaliwa kwa mtoto na hivyo basi ndio wanatarajiwa kuwa msingi na kielelezo bora katika malezi ya mtoto huyu. Ni jukumu la wazazi hawa kufanya na kuongoza mtoto huyu kuzingatia yanayotakikana na jamii yake. Mzazi anapaswa kushawishi mtoto kufuata na kuheshimu mila na desturi za jamii yake. Maadili ya mtoto hadi utu uzima huathiriwa kwa kiasi kikubwa sana na maadili waliyoyashuhudia kutoka kwa wazazi wao. Wazazi ambao hawathamini amani katika familia hukosa mawasiliano miongoni mwao na hata kwa watoto na watoto hawa hukua wakiwa na tabia hii. Imani ni jambo

lingine ambalo mzazi anapaswa kulijenga katika akili na moyo wa mtoto kwamba atakua akimjali Muumba wake. Watoto ambao hawana imani kwa muumba wao hukua wakifanya mambo kwa namna watakavyo bila kujali matokeo ya hatua wanazochukua. Kutokana na maelezo haya, misingi ambayo mzazi anaitia katika moyo na akili ya mtoto, ni dhahiri kuwa mtoto huyu atakua hivyo. Mienendo atakayokuwa nayo katika utu uzima wake ni mwangwi wa mafunzo, maadili na falsafa kutoka kwa wazazi wake.

Kwa upande mwingine, methali *Sikio la kufa halisikii dawa* ni methali ambayo inaweza kutumika kumpigia mfano mtu ambaye unajaribu kumpa maelezo kuhusu faida za kitu fulani lakini anazidi kupuuza tu. Katika hali kama hii, huenda tusiwalaumu wazazi wake kwa malezi yasiyofaa kwani huenda walimwongoza na kumpa mafunzo ya namna anavyopaswa kujiweka kama mwanajamii mwema lakini akawa na misimamo hasi kuhusu mafunzo aliyopata kutoka kwa wazazi wake. Methali hii inaenda sawa na usemi *usishangae mtoto wa Shekhe kuwa Kafiri.* Tumeshuhudia watoto wa viongozi wa dini wakipotoka na wengine kukengeuka na kuchukua mienendo isiyofaa katika jamii. Wengi wa majambazi, kahaba, magaidi na hata washirikina hawakupata malezi kutoka kwa vichochoro. Walikuzwa na viongozi wa dini na wengine wao wakakuzwa katika mazingira ya heshima, utu, ujirani mwema na kila funzo ambalo linaashiria malezi bora. Tabia hizi za kuchukiza walizitoa wapi basi? Swali hili la balagha linaipa methali *Sikio la kufa halisikii dawa* maana yake halisi.

## 4.4 Uchanganuzi wa Jozi za Methali za Kiswahili

Ukinzani wa methali za Kiswahili hujitokeza wakati ambapo kuna jozi ya methali ambazo zina maana zilizo kinyume. Katika mazingira haya, methali moja kutoka kwa jozi hiyo hutoa maana fulani huku nyingine ikitoa maana iliyo kinyume. Kila jamii huwa na mielekeo na maadili ya kuzingatiwa. Mojawapo wa majukumu ya methali ni kuelekeza jamii. Kila mwanajamii ana mguso anaopata kutoka kwa fasihi. Vivyo hivyo, mwanajamii huyu akikabiliana na methali zinazotoa maana iliyo kinyume ni wajibu wake kuamua ni methali gani ambayo itamwongoza kusuluhisha changamoto anayokabiliana nayo au itakayompa mwelekeo unaofaa.

Katika sehemu hii, mtafiti alitoa jozi nane za methali zinazokinzana kwa watafitiwa ambao ni wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne na kuwaomba wachague methali

ambayo inatoa mwelekeo bora kwake yeye binafsi kama mwanajamii na mtumiaji wa lugha ya Kiswahili. Sehemu hii ni muhimu katika utafiti huu kwani matokeo yake yataonyesha wazi msimamo wa jamii kuhusu maisha kwa jumla, utu, bidii, hekima na subira. Kila jozi ya methali zenye maana kinzani ilichanganuliwa na matokeo yake kufasiliwa.

### 4.4.1 Adui mpende/Anipendaye nampenda, anikataaye namkataa

Wanafunzi walitarajiwa kuchagua methali ambayo kila mmoja angependelea itumike katika jamii. Walitarajiwa kufanya uamuzi huu kutoka kwa methali mbili; *adui mpende* na *anipendaye nampenda, anikataaye namkataa*. Jedwali 4.4 lifuatalo linaonyesha matokeo kulingana na uchaguzi kutoka kwa watafitiwa:

**Jedwali 4.4: Adui mpende/Anipendaye nampenda, anikataaye namkataa**

| Jozi 1 | Idadi | Asilimia | Asilimia halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Adui mpende. | 52 | 71.2 | 71.2 | 71.2 |
| Anipendaye nampenda, anikataaye namkataa | 21 | 28.8 | 28.8 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Wanafunzi hamsini na wawili ambao ni asilimia 71.2 walifanya uamuzi kwamba methali inayofaa kutumika katika jamii ni inayoshauri jamii kupenda adui. Kwa upande mwingine wanafunzi ishirini na wawili walichagua methali inayoshauri kumpenda yule akupendaye na kumkataa akukataaye. Hii ni ishara nzuri kwamba hata kizazi cha sasa kinatambua kumtendea mema kila mtu bila kujali iwapo ni adui au rafikiyo.

Waliochagua methali ya kumpenda adui walitoa maelezo kuwa usipompenda adui chuki huzidi na uadui huzidi kutawala miongoni mwenu. Upendo katika jamii huzidisha umoja na maendeleo hupata nafasi nzuri kinyume na wakati ambapo jamii fulani imeamua kuendeleza chuki. Walioshikilia methali ya kupenda akupendaye walitoa sababu kwamba itakuwa upumbavu kuwa mwema kwa mtu ambaye ni adui wa maisha yako. Waliongezea kwamba unapozidi kunyenyekea kwa asiyekupenda,

atakudharau zaidi. Kwamba ni vyema kumpa nafasi anyenyekee kwanza. Wengine walisema kuwa mtu aliye na nia ya kukusaidia ni yule tu anakupenda kwani wasiokupenda watakuzidishia maafa tu.

Jamii halisi ina watu ambao wana maoni tofauti kuhusu suala fulani. Matokeo yanayotokana na jozi hii ni kwamba kuna wanajamii ambao wanashikilia msamaha na wengine ambao kwao, msamaha sio lazima. Idadi kubwa ya watafitiwa katika utafiti huu wanaona umuhimu wa msamaha na kuondoa mawazo yaliyoumbika ndani ya moyo. Hii ni ishara ya kupendeza kubaini kuwa jamii inazingatia sana utu na umoja miongoni mwa wanajamii.

### 4.4.2 Mwenye shoka hakosi kuni/ Penye miti hapana wajenzi

Watafitiwa walipewa methali mbili zilizo na maana kinzani ili kuchagua ile wangependelea itumike katika jamii. Jedwali 4.5 linaonyesha matokeo ya sehemu hii:

**Jedwali 4.5: Mwenye shoka hakosi kuni/ Penye miti hapana wajenzi**

| Jozi 2 | Idadi | Asilimia | Asilimia halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Mwenye shoka hakosi kuni | 61 | 83.6 | 83.6 | 83.6 |
| Penye miti hapana wajenzi | 12 | 16.4 | 16.4 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Wanafunzi sitini na mmoja walioshiriki katika utafiti huu walichagua methali *Mwenye shoka hakosi kuni* huku wanafunzi kumi na wawili wakichagua methali *Penye miti hapana wajenzi* zitumike katika jamii, mtawalia.

Shoka ni kifaa ambacho hutumika kukatia miti au kuchanjia kuni. Methali *mwenye shoka hakosi kuni* ina maana kuwa anayemiliki kifaa hiki hana budi kuwa na kuni katika boma lake. Kuni zina kazi tofauti katika jamii; zinaweza kutumika kuchomwa motoni ili kupikia au zikatumika kupasha nyumba moto. Kutokana na kauli hii basi, aliye na kuni hizi hatatatizika wakati wa mapishi na pia nyakati za baridi, nyumba yake itakuwa na kiwango cha joto inayofaa. Asiye na kifaa shoka ambacho hukipata

kwa kuombaomba huenda akakosa manufaa haya kwani kuni chache alizo nazo anazipima tu labda kwa kuhofia huenda akakosa shoka atakapolihitaji.

Kwa upande mwingine, methali *penye miti hapana wajenzi* ina maana kwamba mara nyingi palipo na nyenzo nyingi hapana wenye maarifa ya kupaendeleza. Hii ni methali inayotumiwa kwa wanajamii ambao mazingira yao yamejaa vitu ambavyo vinaweza kuwafaidi lakini hawajachukua fursa au hata mawazo ya kujifaidi kutoka kwavyo. Katika maisha halisi ya sasa, sio ajabu kupata watu ambao wanalia na kulaumu umaskini ilhali wamekalia maarifa na malighafi ambayo yanaweza kuwafungulia milango ya kujipatia riziki na zaidi utajiri. Tumeshuhudia vijana wengi ambao wamesoma na vyeti wanavyo lakini wamevitia mifukoni na kulaumu uongozi kwa kutowapa kazi. Ajabu ni kwamba wale ambao hawana hata cheti kimoja cha kiakademia wanatia bidii kujitajirisha kwa kuanzisha vibiashara ambavyo vinakua na kuwaletea mwangaza kifedha.

Maoni ya watafitiwa ni kwamba methali inayoshawishi wanajamii kutia bidii katika shughuli zao za kila siku inapaswa itumike na sio inayowadhalilisha na kuzima ndoto zao za usoni. Asilimia kubwa ya walioshiriki utafiti ni kwamba methali *mwenye shoka hakosi kuni* inapaswa kutumika ili kuhakikisha kwamba maendeleo katika jamii yanadhihirika. Waliochagua methali ya pili walidai kuwa watu wengi wamekosa maono kuhusu maisha yao na hawataki kujifanyia kazi kwa kutumia vichache walivyo navyo. Kwa hivyo wanapaswa kutajiwa methali hii ili wajue namna watakavyochangamka na kupanga siku zao za usoni.

### 4.4.3 Nahodha wengi chombo huenda mrama/Panapo wengi hapaharibiki jambo

Katika jamii kuna aina mbili za watu kulingana na methali katika jozi hii. Wapo wanaoshikilia umoja huku wengine wakiwa na msimamo wa kujitegemea katika shughuli zao za kila siku. Kila mtafitiwa alitarajiwa kuchagua methali ambayo kulingana naye inafaa kutumiwa na jamii. Jedwali 4.6 lifuatalo linaonyesha matokeo ya utafiti:

**Jedwali 4.6: Nahodha wengi chombo huenda mrama/Panapo wengi hapaharibiki jambo**

| Jozi 3 | Idadi | Asilimia | Asilimia halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Nahodha wengi chombo huenda mrama | 24 | 32.9 | 32.9 | 32.9 |
| Panapo wengi hapaharibiki jambo | 49 | 67.1 | 67.1 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Idadi ya waliochagua methali, *Nahodha wengi chombo huenda mrama* ni watafitiwa ishirini na wanne ikiwa asilimia 32.9 huku waliochagua methali *Panapo wengi hapaharibiki jambo* wakiwa arobaini na tisa, asilimia 67.1. Matokeo haya yanasawiri jamii ambayo imekubali kushirikiana katika shughuli zao ziwe za jamii au za mtu binafsi.

*Nahodha wengi chombo huenda mrama* ina maana kwamba wakati ambapo waelekezi ni wengi, huenda mambo yakaharibika. Inatoa shinikizo kuwa wingi wa wahusika katika utekelezaji shughuli fulani husababisha kusambaratika kwa mambo. Labda kutokana na maoni na mawazo tofautitofauti ambayo huenda yakazua fujo haswa iwapo kila mmoja anajiona kama mjuzi wa kinachotekelezwa au kinachozungumziwa. Kwa upande mwingine, methali panapo wengi hapaharibiki jambo inashauri jamii kuwa na ushirikiano na umoja wanapotekeleza mambo kama jamii au hata mambo yao binafsi. Waliochagua methali hii walitetea msimamo wao kwa madai kuwa watu wakifanya jambo kwa pamoja kazi hiyo huwa na mwisho mzuri na wa kuvutia macho. Maoni na mawaidha yanayotolewa na kila mhusika huwa ya manufaa katika shughuli hiyo iwapo yatachukuliwa kwa mwelekeo wa kujenga na sio wa kuharibu.

Msimamo waliotoa watafitiwa katika utafiti huu ni kwamba wameshuhudia mazuri yanayotokana na umoja miongoni mwa wanajamii na pia madhara yaliyo katika maisha ya wanajamii ambao wanaamini sana kujitegemea wao wenyewe katika kutekeleza shughuli zao. Kutokana na maoni yao, jamii yao imewakilishwa kama jamii ambayo inachukia utengano na kukumbatia utangamano. Jamii ambayo ina ushirikiano mambo yake husonga kwa mwendo wa kasi na hatima yake huwa ya

kupendeza kwani kila mmoja anaelewa majukumu yake na huyatekeleza kama anavyotarajiwa.

### 4.4.4 Akutendaye ubaya mlipe kwa wema/ Akutendaye mtende

Katika harakati za kutangamana na wanajamii wenzetu, mambo yaliyo na uwezo wa kuharibu uhusiano mwema hutokea. Jozi hii ya methali ina mielekeo miwili; wa kwanza ukiwa unashauri kulipa mabaya kwa mema na mwelekeo wa pili ukishauri kulipiza kisasi. Kila mwanafunzi alitakiwa kuchagua mwelekeo ambao anahisi kwamba unapaswa kuiongoza jamii. Jedwali 4.7 linaonyesha matokeo kuhusu mielekeo ya wanafunzi waliotafitiwa:

**Jedwali 4.7: Akutendaye ubaya mlipe kwa wema/ Akutendaye mtende**

| Jozi 4 | Idadi | Asilimia | Asilimia halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Akutendaye ubaya mlipe kwa wema | 52 | 71.2 | 71.2 | 71.2 |
| Akutendaye mtende | 21 | 28.8 | 28.8 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Wanafunzi hamsini na wawili ambao ni asilimia 71.2 walichagua mwelekeo unaoshawishi jamii kulipa mabaya kwa mema huku wanafunzi ishirini na mmoja ambao ni asilimia 28.8 wakichagua mwelekeo wa kulipiza kisasi kwa wanaokutendea mabaya.

Baadhi ya waliochagua mwelekeo wa kusamehe wanaokutendea mabaya wanaamini kuwa hata Mungu atakulipa kulingana na mema unayowafanyia wengine. Walichokisisitiza ni kwamba sio vyema kulipiza kisasi kwani unapofanya hivi, utajenga chuki ambayo huenda ikaleta madhara yasiyotarajiwa na zaidi unajikoseshea amani moyoni mwako. Waliochagua methali ya kumtenda akutendaye walitetea msimamo wao kwamba kuna watu ambao mara nyingi hujifanya marafiki wa karibu lakini matendo yao yanaonyesha uadui kwa uwazi sana. Unapozidi kupuuza matendo hayo na kujifanya mzuri kwa kulipiza mema, watakuona ovyo na mtu asiyekuwa na akili kwani hupambanui matendo bali unasikiza na kufuata maneno tu.

Matokeo ya sehemu hii ni sawa na matokeo ya jozi ya kwanza. Hii ni ishara kwamba watafitiwa ambao (katika jozi ya kwanza) walichagua methali ya *Adui mpende*, walizidi kushikilia msimamo wao wa kuhakikisha kwamba amani inatamalaki katika jamii na wakachagua methali *Akutendaye ubaya mlipe kwa wema*. Kinachobainika kutokana na utafiti huu ni kwamba wapo wanajamii wachache ambao kulingana nao, hupaswi kumruhusu mtu akutende kisha "umwache hivyo tu" - lazima nawe umtende ili labda moyo wako utosheke. Hata hivyo idadi kubwa ni ya wale ambao kulingana nao kilicho muhimu zaidi ni kutafuta baraka kwa kuachilia uchungu uliopata kutoka kwa mwenzake na kuzidi kutenda mema kwa kila mja bila kujali urafiki au uadui.

### 4.4.5 Fuata nyuki ule asali/Fuata nyuki ufie mzingani

Kila mtu ana malengo yake kama mwanajamii na kama mtu binafsi. Changamoto tunazokabiliana nazo ili kuyafikia si haba. Methali zinatoa mwelekeo wa kuongoza jamii katika kutimiza ndoto zao maishani. Katika sehemu hii, wanafunzi walitarajiwa kuchagua methali ambayo kwa maoni yao inapaswa kuelekeza jamii ili kufikia malengo yake. Jedwali 4.8 lifuatalo linaonyesha matokeo ya utafiti huu.

**Jedwali 4.8: Fuata nyuki ule asali/Fuata nyuki ufie mzingani**

| Jozi 5 | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Fuata nyuki ule asali | 53 | 72.6 | 72.6 | 72.6 |
| Fuata nyuki ufie mzingani. | 20 | 27.4 | 27.4 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Kwa mujibu wa matokeo katika sehemu hii, asilimia 72.6 walichagua methali fuata nyuki ule asali huku asilimia 27.4 wakichagua methali fuata nyuki ufie mzingani.

Katika methali ya kwanza, maneno nyuki na asali yametumiwa kama ishara. Nyuki ni mdudu ambaye huishi mzingani na hutengeneza asali ambayo huthaminiwa sana na watu wengi. Mojawapo ya njia za kujua palipo na mzinga ni kufuata nyuki hawa ambao huishi pamoja katika kikundi, aghalabu mzingani. Ukishapata ule mzinga basi una hakikisho la kupata asali na utafurahia utamu wake. Methali hii inashauri kuwa vitu vya thamani hupatikana kutokana na juhudi za anayekihitaji, King'ei (1989).

Kwa upande mwingine methali fuata nyuki ufie mzingani inatoa maana kinyume na ile ya kwanza kwamba nyuki pia wana sifa ya kuuma na ukivamiwa na kikundi kizima cha nyuki bila shaka kuna uwezekano mkubwa wa kupatana na mauti pale. Ushauri unaotolewa na methali hii ni onyo kwa walio na matamanio fulani kwamba wajue kuwa japo unachokifuata kina manufaa yake, kinaweza kukupa maafa au madhara ambayo yatachukua muda kusahaulika. Ukipigiwa methali hii utapatwa na uoga wa kufuata ndoto zako kwa kuhofia changamoto utakazokumbana nazo huku ukisahau manufaa ya kufikia malengo yako.

Matokeo ya utafiti huu yanashamiri jamii ambayo kwayo, wanachokithamini ni kufuata malengo yao maishani labda wakiwa na majibu au suluhu ya changamoto watakazokabiliana nazo safarini. Idadi chache ya watafitiwa inawakilisha baadhi ya wanajamii ambao wana uoga wa maisha. Si ajabu kushuhudia mtu ambaye anatamani kufikia malengo fulani lakini kutokana na hofu za asichokuwa na habari nacho anakata tamaa na kukubali kuishi katika hali duni tu.

### 4.4.6 Mavi ya kale hayanuki/Mavi ya kale hayaachi kunuka

Maovu yanapotokea katika jamii, huwa yanatekelezwa na mtu au kikundi cha watu katika jamii hiyo. Kama wanajamii, tuna jukumu la kusamehe aliyetenda hayo au kutomsamehe. Baada ya matukio hayo, aliyetekeleza maovu hayo hupata picha fulani kutoka kwa wanajamii, kuhusu tabia yake. Katika sehemu hii watafitiwa walitarajiwa kuchagua mwelekeo walionao kuhusu tabia ya mtu. Jedwali 4.9 lifuatalo linaonyesha matokeo ya utafiti huu:

**Jedwali 4.9: Mavi ya kale hayanuki/Mavi ya kale hayaachi kunuka**

| Jozi 6 | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Mavi ya kale hayanuki | 33 | 45.2 | 45.2 | 45.2 |
| Mavi ya kale hayaachi kunuka. | 40 | 54.8 | 54.8 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Watafitiwa thelathini na watatu ambao ni asilimia 45.2 walichagua methali *mavi ya kale hayanuki* huku watafitiwa arobaini, asilimia 54.8 wakichagua methali *mavi ya kale hayaachi kunuka*. Idadi kubwa ya watafitiwa ina mwelekeo kuwa tabia za mtu kamwe hazimwachi.

Neno ‘mavi’ limetumika katika methali hizi kama ishara tu. Linaweza kumaanisha tabia au mwenendo wa mtu au hata jamii fulani. Methali *mavi ya kale hayanuki* ina maana kwamba tabia au mienendo ya mtu ya zamani haiwezi kutumika kutoa hukumu kumhusu. Upo uwezekano wa mtu kubadilika na kuacha mienendo yake isiyofaa na kuwa mtu mwema. Kwa upande mwingine, methali mavi ya kale hayaachi kunuka ina maana kwamba tabia ya mtu ni ya mtu na hawezi kuiacha kamwe. Picha inayohifadhiwa katika akili za wanajamii kuhusu mtu mahususi huhusishwa na matendo mazuri au mabaya aliyoyatenda hapo awali.

Waliochagua methali ya kwanza walitetea msimamo wao kwa kusema kuwa ni vyema kusahau na kusamehe mabaya uliyotendewa hapo awali. Walisisitiza kuwa sio haki kuhukumu leo ya mtu kwa kutumia mabaya aliyoyatenda hapo jana kwani kuna nafasi ya mwanajamii huyo kubadilika na kuacha mienendo yake isiyofaa. Kwa upande mwingine waliochagua mwelekeo unaoletwa na methali mavi ya kale hayaachi kunuka walitetea kauli yao na kusema kuwa ni jukumu la kila mwanajamii kujitolea kutenda mema kwani uovu hausahauliki kamwe. Kwamba mabaya unayofanya yanaendelea kujenga historia yako na hivyo ndivyo jamii itakavyokuchukulia. Hata ukibadilika, madhara yaliyosababishwa na maovu yako yatabaki katika maisha ya aliyeathiriwa na kitendo hicho.

Matokeo ya sehemu hii yanaonyesha wazi kwamba mara nyingi kesho ya mtu hujengwa na aliyoyatenda hapo awali. Ingawa watu wanaweza wakakusamehe, ubaya uliotenda utabaki katika akili zao na hivyo ndivyo utakavyoonekana kila mara hata baada ya kukiri kwao kwamba umebadilika.

### 4.4.7 Ngoja ngoja huumiza matumbo/Mstahimilivu hula mbivu

Katika sehemu hii mtafiti alilenga kujua msimamo wa watafitiwa kuhusu suala la kuvumilia na kusubiri hadi muda uruhusu mambo fulani kutimia maishani mwake. Kila mwanafunzi alitakiwa kuweka alama ya vema karibu na methali ambayo kulingana naye, inapaswa itumike katika jamii. Matokeo ya sehemu hii yameonyeshwa na jedwali 4.10 lifuatalo:

| **Jozi 7** | **Idadi** | **Asilimia** | **Asilimia Halisi** | **Asilimia Jumuishi** |
|---|---|---|---|---|
| Ngoja ngoja huumiza matumbo | 19 | 26 | 26 | 26 |
| Mstahimilivu hula mbivu | 54 | 74 | 74 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Kati ya watafitiwa waliohusika, wanafunzi hamsini na wanne ikiwa ni asilimia 74 walichagua methali *mstahimilivu hula mbivu* huku wanafunzi kumi na tisa, asilimia 26 wakichagua methali *ngoja ngoja huumiza matumbo.*

*Ngoja ngoja huumiza matumbo* ni methali ambayo inashauri wanajamii kusubiri kwingi hakuna manufaa kwani hatima yake ni kuleta uchungu, kutofikia malengo na maumivu kwa anayesubiri. Waliochagua methali hii walijitetea kwa kusema kuwa sio vyema kuketi tu na kusubiri kupata suluhu kutoka kwa mtu au namna moja tu ilhali kuna njia nyingi za kupata suluhu hiyo. Wengine walisema kuwa kusubiri ni njia ya kupoteza muda tu; jibu au suluhu hutafutwa na kwa hivyo badala ya kusubiri, mtu anapaswa kupata njia mbadala ya kumpa suluhu hiyo. Idadi kubwa ya watafitiwa walichagua methali *mstahimilivu hula mbivu* na kutetea msimamo wao kwa kusema kwamba hakuna haja ya kuwa na papara wakati unataka kufanya jambo fulani. Ni vyema mtu au jamii isiwe ya kukata tamaa bali iwe na uvumilivu hadi tamati kwani mambo yatakuwa mazuri bila shaka. Wengi walitumia methali tofauti tofauti kutetea msimamo wao, kwa mfano simba mwenda pole ndiye mla nyama na haraka haraka haina baraka.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, ni ishara tosha kwamba jamii iliyohusika katika utafiti huu ni jamii ambayo inazingatia sana mwenendo wa kuwa na subira katika kila

jambo. Uvumilivu ni neno la kawaida katika akili za wengi lakini ni wachache tu ambao wana tabia hii. Jamii ya sasa ina tamaa ya kufikia malengo yake kwa haraka haswa vijana ambao kwao utajiri ndio maisha bora. Kutokana na imani hii wengi wanautafuta kwa vyovyote vile hata kutumia njia za kuzimuni, ugaidi na hata kuuza dawa za kulevya. Jamii kama hii inapaswa kusisitiziwa maana na umuhimu wa methali *Mstahimilivu hula mbivu.*

### 4.4.8 Adhihakiye kovu hajaona jeraha/Achekaye kilema na kwao kipo

Maisha tunayoishi kila siku yamejaa sifa za ulemavu wa aina tofauti; kupungukiwa, umaskini, ujinga na kadhalika. Kuna walio navyo na wasiokuwa navyo, na wote ni wanajamii. Mara nyingi walio na neema ya kuishi vyema hukosa utu na kuwadhihaki waliokosa neema hiyo. Kutokana na uhalisi huu wa mambo mtafiti alitaka kujua kutoka kwa watafitiwa wake ni methali gani inayofaa kutumiwa na wanajamii. Matokeo ya sehemu hii yanaonyeshwa na jedwali 4.11 kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.11:Adhihakiye kovu hajaona jeraha/Achekaye kilema na kwao kipo**

| Jozi 8 | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Adhihakiye kovu hajaona jeraha | 28 | 38.4 | 38.4 | 38.4 |
| Achekaye kilema na kwao kipo | 45 | 61.6 | 61.6 | 100 |
| **Jumla** | **73** | **100** | **100** | |

Wanafunzi ambao walichagua methali *Adhihakiye kovu hajaona jeraha* ni asilimia 38.4 huku asilimia 61.6 wakachagua methali *Achekaye kilema hata kwao kipo*.


Methali *adhihakiye kovu hajaona jeraha* hutumika kutoa kejeli kwa watu ambao huwacheka na kuwadhihaki wanajamii ambao wanapitia changamoto fulani katika maisha yao. Neno 'kovu' limetumika kuashiria mapito, tatizo au hata ulemavu alio nao mwanajamii fulani. Mara nyingi huwa hatuelewi watu wa aina hii na hata hufikia wakati tunawadharau na kuwalaumu kwa wanayopitia kwa sababu hayajatufika na

hivyo hatujui uchungu wanaokabiliana nao. Kwa upande mwingine methali *achekaye kilema na kwao kipo* inalenga wanajamii ambao wanawadhihaki na kuwacheka walio na changamoto fulani maishani mwao kutokana na sababu kwamba labda wanapitia changamoto hiyo ama waliwahi kuipitia. Ukinzani unajitokeza katika methali hizi kwamba aliye na kovu unamcheka kwani hujapitia hayo huku ya pili ikiwa na maana kuwa unamdhihaki kilema kwani hata kwenu au kwako ulemavu huo upo.

### 4.5 Umuhimu wa Ukinzani Katika Methali za Kiswahili

Katika sehemu hii, utafiti huu ulilenga kujua kutoka kwa wanafunzi walioshiriki katika zoezi hili iwapo kwa maoni yao kuna haja ya kuwa na methali zinazoleta maana kinyume katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Watafitiwa walitakiwa kuchagua jibu ndio au la na kutoa maelezo mafupi sana kuhusu uamuzi wao. Matokeo yao yameonyeshwa katika mchoro 4.12 ufuatao:

**Mchoro 4.12 unaoonyesha matokeo kuhusu umuhimu wa ukinzani katika methali za Kiswahili.**




Wanafunzi arobaini na sita ambao ni asilimia 63 walisema kuwa kuna haja ya kuwa na methali kinzani katika lugha ya Kiswahili huku watafitiwa ishirini na saba ambao ni asilimia 37 walisema kwamba hakuna haja ya kuwa na methali kinzani katika lugha ya Kiswahili.

Watafitiwa waliochagua umuhimu wa kuwepo na methali kinzani katika fasihi ya Kiswahili walitetea msimamo wao na kusema kwamba methali kinzani zinasaidia jamii kutafakari kabla ya kuchagua mwelekeo wa kufuata na kuepuka njia ambayo ingewaletea matatizo baadaye. Wengine walisema kuwa kila methali ina maana yake na ukinzani huu huja tu tukianza kulinganisha maana za methali. Kwa hivyo, kinachopaswa kutuongoza ni maana ya methali kulingana na mazingira ya matumizi na sio kulinganisha. Ulinganishaji huu unaweza kupotosha mtu. Watafitiwa wengine walisema kuwa methali zinapokinzana zinasaidia wanajamii kuangalia pande zote mbili; zuri na baya na kisha kufanya uamuzi kutegemea falsafa yao kuhusu masuala yanayopatikana katika jamii yao. Kila methali katika jozi zilizo na ukinzani huwakilisha hali halisi ya jamii. Kwamba, kuna methali moja inayopotosha huku nyingine ikielekeza jamii kuliko kwema.

Waliosema hakuna haja ya methali kinzani katika lugha ya Kiswahili walitetea msimamo wao kwa kutoa kauli kuwa ukinzani huleta utata na ugumu wa kuelewa maana na matumizi ya methali. Baadhi yao walikiri kuwa hakuna haja ya kuwa na methali moja inayotoa maana fulani na nyingine inajitokeza na kutoa maana kinyume kuhusu suala moja tu. Huku ni kupoteza maana asilia ya methali.

### 4.6 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Ukinzani Katika Methali za Kiswahili

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kubaini mielekeo walio nayo wanafunzi kuhusu suala la methali za Kiswahili zenye maana kinyume. Utafiti ulidhamiria kujua iwapo wanafunzi wana mwelekeo chanya au hasi. Kila mwanafunzi alitakiwa kutoa msimamo wake na kutoa maelezo mafupi kuhusu msimamo aliochagua. Mchoro 4.13 unaonyesha matokeo ya sehemu ya utafiti huu.

**Mchoro 4.13: Unaoonyesha matokeo ya wanafunzi kuhusu mielekeo yao kuhusu methali kinzani.**




Kwa mujibu wa matokeo ya sehemu hii ya utafiti, ilibainika kwamba asilimia 47 ya watafitiwa walisema kuwa ukinzani katika methali za Kiswahili huleta mwelekeo hasi huku asilimia 53 wakisema ukinzani huleta mwelekeo chanya miongoni mwa watumiaji lugha.

Waliosema methali kinzani huleta mwelekeo chanya walitetea msimamo wao kwamba ukinzani katika methali za Kiswahili huleta sura zote za jamii. Kwamba methali hizi hutoa uhalisi wa mambo yanayoathiri maisha ya mwanadamu. Kila methali hutoa maana iliyo na ukweli fulani kutegemea mazingira ya matumizi. Methali kinzani hutoa mwongozo kwa mambo tofauti katika jamii. Kila methali katika jozi ya methali zenye maana kinzani huwa na ujumbe kwa hadhira. Kwa mfano, ujumbe wa kujenga urafiki au kuendeleza uadui. Tukiangalia jozi ya methali; *adui mpende* na *Anipendaye nampenda anikataaye nami namkataa*, methali ya kwanza inashawishi jamii kuendeleza uhusiano mwema huku ya pili ikipotosha jamii kwamba wa kuenziwa ni anayekuenzi!

Watafitiwa wengine walitoa maoni kuwa ukinzani katika fasihi ya Kiswahili ni mojawapo wa nyenzo za kupamba lugha na fasihi. Lugha ya fasihi haipaswi kuwa lugha kavu na kwa hivyo, methali kinzani huchangia katika kuhakikisha kwamba

zimeongeza ladha katika lugha hii. Vilevile, watumiaji lugha wanapoendelea kufafanua maana na matumizi ya methali kinzani na hata kutafuta jozi za methali za Kiswahili zilizo na maana kinzani huwa wanakuza ubunifu wao wa kufikiria na zaidi kupevua akili zao. Maoni mengine yaliyotolewa ni kwamba pale ambapo kuna methali ambayo ina maana inayopotosha, kuna uwezekano wa kupata methali nyingine inayotoa mwelekeo usio wa kupotosha.

Watafitiwa walio na mwelekeo hasi kuhusu methali kinzani walitetea msimamo wao kwa madai kuwa mara nyingi ni vigumu sana kutumia methali kama njia ya kumpa mwanajamii fulani mwongozo kuhusu suala fulani kwani atatumia methali inayotoa maana kinyume kukosoa mawaidha yako. Wengine walisema kuwa methali kinzani hutoa maana inayochanganya na kutatanisha akili za wanajamii. Kwamba methali moja inatoa mwelekeo fulani na nyingine inajitokeza kupinga mwelekeo huo.

Matokeo ya utafiti ni kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa ina mwelekeo chanya kuhusu ukinzani katika methali za Kiswahili. Kila methali hubeba maana yake iliyo na ukweli na mwongozo fulani kwa wanajamii. Iwapo jamii itatumia methali katika mazingira mahususi, ukinzani katika methali hautajitokeza. Maoni haya yanaoana na msimamo wa Yankah (1994) kuhusu suala la ukinzani katika lugha.

### 4.7 Uchanganuzi wa Data Kutoka kwa Walimu

Data iliyokusanywa kutoka kwa walimu itachanganuliwa katika sehemu hii. Sehemu ya kwanza itaangazia habari za kimsingi za watafitiwa ambazo ni pamoja na jinsia, tajriba yake kama mwalimu na kama mwalimu wa fasihi, kidato anachofunza na pia utahini wa fasihi ya Kiswahili kitaifa.

#### 4.7.1 Habari za Kimsingi

Data inayohusiana na mambo binafsi ya walimu ni muhimu katika utafiti huu. Kutokana na habari mwalimu mahususi atakazotoa, mtafiti ataweza kufahamiana kwa namna fulani na mtafitiwa wake.

#### 4.7.2 Jinsia ya mtafitiwa.

Sehemu hii ililenga kubaini jinsia ya walimu waliohusika katika utafiti. Mtafiti aliwaomba kutaja jinsia yao. Matokeo yanaonyeshwa na jedwali 4.14:

**Jedwali 4.14: Jinsia ya mtafitiwa**

| Jinsia | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Kiume | 6 | 40 | 40 | 40 |
| Kike | 9 | 60 | 60 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **15** | **100** | |

Matokeo yanayohusiana na sehemu ya jinsia ya mtafitiwa yanadhihirisha kwamba watafitiwa wa kike wana asilimia kubwa ikilinganishwa na ile ya walimu wa jinsia ya kiume. Asilimia 60 ya watafitiwa ilikuwa ya jinsia ya kike huku walimu wa kiume wakiwa 40. Kutokana na hili uwezekano wa kisio kwamba idadi kubwa ya walimu wanaofunza fasihi ya Kiswahili katika shule za upili eneo la Kitui mjini ni ya jinsia ya kike, linajitokeza.

Mtafiti alijumuisha jinsia zote mbili kama sampuli yake ili kuhakikisha kwamba maoni yanayotoka kwa watafitiwa yana usawa wa kijinsia; kwamba kila jinsia imewakilishwa ipasavyo katika utafiti huu ambao unahusiana sana na fasihi inayofundishwa katika kiwango cha shule ya upili. Usawa wa kijinsia ni jambo ambalo kila jamii inapaswa kutilia maanani kwa sababu maeneo ambayo yana usawa huu huweza kuwa na mafanikio mengi na bora zaidi ikilinganishwa na wale ambao wanaheshimu jinsia moja na kupuuza nyingine.

### 4.7.3 Tajriba Kama Mwalimu Katika Shule ya Upili

Mtafiti alitaka kujua muda ambao mtafitiwa ameweza kufanya kazi kama mwalimu wa shule ya upili kwa jumla. Watafitiwa walitakiwa kuweka alama ya vema karibu na jibu walilochagua. Jedwali 4.15 linaonyesha matokeo:

**Jedwali 4.15: Tajriba kama mwalimu katika shule ya upili**

| Tajriba | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Miaka 15 na zaidi | 1 | 6.7 | 6.7 | 6.7 |
| Miaka 10-15 | 1 | 6.7 | 6.7 | 13.3 |
| Miaka 5-10 | 3 | 20 | 20 | 33.3 |
| Miaka 0-5 | 10 | 66.7 | 66.7 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **100** | |

Matokeo katika sehemu hii yanatoa ishara kwamba asilimia 66.7 ya watafitiwa wamefundisha katika shule ya upili kwa muda wa kati ya miaka 0-5, asilimia 20 kati ya miaka 5-10, asilimia 6.7 kati ya miaka 10-15 huku asilimia 6.7 wakiwa wamefundisha kwa miaka 15 na zaidi. Idadi ya watafitiwa 10 kati ya watafitiwa 15 ni asilimia kubwa.

Kati ya walimu 15 waliotafitiwa, ni walimu wawili tu ambao wamefanya kazi ya ualimu kwa zaidi ya miaka kumi. Hii ina maana kwamba wengi wa watafitiwa hawa wana tajriba ya kiwango cha chini katika masuala ya fasihi. Itakuwa bora zaidi iwapo tafiti za usoni zitakazofanywa zitahusisha idadi kubwa ya walimu ambao wamekuwa katika uwanja wa ualimu kwa miaka mingi.

### 4.7.4 Tajriba Kama Mwalimu wa Fasihi ya Kiswahili

Katika sehemu hii mtafiti alikuwa na nia ya kujua idadi ya miaka ambayo mtafitiwa wake ameweza kusomesha fasihi ya Kiswahili. Matokeo katika sehemu hii ni tofauti na ya sehemu ya 4.7.3. Kinachozingatiwa hapa ni tajriba ya mwalimu wa fasihi ya Kiswahili na sio mwalimu wa shule ya upili kwa jumla. Jedwali 4.16 lina matokeo:

**Jedwali 4.16: Tajriba kama mwalimu wa fasihi ya Kiswahili**

| Tajriba | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Miaka 15 na zaidi | 1 | 6.7 | 6.7 | 6.7 |
| Miaka 10-15 | 1 | 6.7 | 6.7 | 13.3 |
| Miaka 5-10 | 3 | 20 | 20 | 33.3 |
| Miaka 0-5 | 10 | 66.7 | 66.7 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **100** | |

Kati ya walimu kumi na tano waliotafitiwa, walimu kumi wana tajriba ya kati ya miaka 0-5, walimu watatu wakiwa na tajriba ya miaka 5-10, mwalimu mmoja kati ya miaka 10-15 na mwalimu mwingine akiwa na tajriba ya miaka 15 na zaidi.

Matokeo haya yanaashiria kuwa kwa kuzingatia muda ambao mwalimu amefundisha fasihi ya Kiswahili, idadi kubwa ya watafitiwa ina tajriba ya miaka machache katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili. Tafiti za usoni zinazohusiana na utafiti huu zinaweza kukusanya data kutoka kwa walimu ambao wana tajriba ya miaka mingi katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili.

### 4.7.5 Kidato Anachosomesha Mwalimu

Mtafiti alitaka kujua kidato ambacho mwalimu mahususi anachosomesha fasihi ya Kiswahili. Mwalimu ambaye anaingiliana na wanakidato cha nne ana nafasi ya kuingiliana na fasihi ya Kiswahili kwa undani na upana kwani wanafunzi hawa wamekomaa kiakili na mawazo yao yamepevuka ikilinganishwa na wanafunzi wa vidato vya chini. Watafitiwa walitakiwa kuweka alama ya vema karibu na jibu walilochagua. Jedwali 4.17 linaonyesha matokeo ya sehemu hii.

**Jedwali 4.17: Kidato Anachosomesha Mwalimu**

| Kidato | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Cha 3 | 7 | 46.7 | 46.7 | 46.7 |
| Cha 4 | 8 | 53.3 | 53.3 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **100** | |

Baada ya uchanganuzi wa data ya walimu kuhusu kidato mwalimu mahususi anachofundisha, ilibainika kwamba asilimia kubwa ya walimu wanafundisha kidato cha nne. Asilimia 53.3 ni ya walimu wa kidato cha nne huku asilimia 46.7 ikiwa ya walimu wa kidato cha tatu. Tofauti hii sio pana ishara kwamba walimu wa vidato hivi viwili walipewa haki sawa kutoa maoni na mielekeo yao kuhusu suala lililokuwa likifanyiwa utafiti.

### 4.7.6 Utahini wa Fasihi ya Kiswahili

Katika sehemu hii mtafiti alidhamiria kujua iwapo mtafitiwa wake amefikia kiwango cha kutahini fasihi ya Kiswahili katika mitihani ya kitaifa. Mwalimu ambaye anatahini mtihani huu ana nafasi bora zaidi ya kuingiliana na fasihi ya Kiswahili. Mtafitiwa aliombwa kuonyesha iwapo anatahini fasihi ya Kiswahili au la. Matokeo yanaonyeshwa na jedwali 4.18:

**Jedwali 4.18: Tajriba ya mwalimu kama mtahini wa fasihi ya Kiswahili**

| Utahini | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Ndio | 6 | 40 | 40 | 40 |
| La | 9 | 60 | 60 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **400** | |

Walimu ambao wana jukumu la kutahini mitihani ya kitaifa hupata nafasi ya kipekee ya kutangamana na fasihi ya Kiswahili. Utangamano huu huchangia katika kupanua mawazo na maarifa yao kuhusiana na fasihi na lugha. Asilimia kubwa ya walimu waliohusika katika utafiti huu imechukuliwa na wale ambao hawajafikia kiwango cha

kutahini fasihi ya Kiswahili. Asilimia 40 ni ya wanaotahini huku asilimia 60 ikiashiria nafasi ya wale ambao si watahini.

### 4.8 Uchanganuzi wa Data Inayohusiana na Mada ya Utafiti

#### 4.8.1 Namna Ukinzani Unavyojitokeza Katika Baadhi ya Methali za Kiswahili

Maana ya msingi ya neno ukinzani ni ubishi au ushindani. Methali za Kiswahili zina sifa ya kuwa na baadhi ya jozi ambazo zinatoa maana zilizopingana. Mtafiti aliwapa walimu wa fasihi ya Kiswahili swali la kutaja mifano ya methali za Kiswahili zilizo na ukinzani kama njia ya kuwachangamsha akili. Wengi wao walitoa methali ambazo tayari zimechanganuliwa katika sura ya kwanza na ya pili ya utafiti huu. Jozi za methali zitakazochanganuliwa katika sehemu hii ni zile tu hazijachanganuliwa tayari ili kuzuia kujirudia.

##### 4.8.1.1 Kuuliza si ujinga/ Asiyejua maana haambiwi maana

Maana ya juu ya methali '*kuuliza si ujinga*' ni kuwa mtu anapotoa swali kuhusu jambo fulani hapaswi kuchukuliwa kana kwamba yeye ni mjinga. Maana ya ndani ni kuwa ili kupata maarifa kuhusu suala fulani, kuuliza na kupata jibu kutoka kwa anayefahamiana na jambo hilo ni njia ya kujipatia suluhisho au ujuzi. Methali hii inamhimiza mtumiaji lugha kutojionea soni anapouliza kuhusu asichokifahamu. Ni jukumu lake kupata ufahamu kutokana na kuuliza.

Methali ya pili nayo ina maana kuwa iwapo hauna habari kuhusu kinachozungumziwa basi haupaswi kuambiwa maana yake na yeyote yule. Methali hii inatoa ushauri kwa wanajamii kuwa mtu hapaswi kujitia aibu kwa kuuliza kupata maana au uelewa wa jambo fulani kwani hataambiwa.

Ukinzani katika methali hizi mbili unadhihirika kwa njia iliyo wazi. Methali ya kwanza inampa mwanajamii mwelekeo wa kutafuta habari au maarifa kwa njia ya kuuliza kutoka kwa watu au jamii. Kwa upande mwingine methali ya pili nayo inamwelekeza mwanajamii huyu upande wa kujiwekea yale ayajuayo na pia asiyojua kwani hata akitafuta jibu kuyahusu hatalipata. Hali kama hii humfanya mwanajamii kukanganyikiwa na mambo asijue ni njia gani ya kufuata. Atakosa uhakika kwamba iwapo atafanikiwa kupata jibu la swali lake au atabezwa tu.

#### 4.8.1.2 Ukitaka kumla nguruwe chagua aliyenona/ Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti

Nguruwe ni mnyama anayefugwa, mnene na mfupi na mwenye pua kubwa. Waislamu huamini kuwa nyama ya mnyama huyu ni haramu. Nyama yake hupendwa sana na baadhi ya watu. Mara nyingi tunapohitaji kumchinja mnyama ili kupata kitoweo huwa tunajipata tukimchagua yule ambaye amenona. Macho huongoza katika kufanya uamuzi huu. Methali hii inatoa ushauri kwamba uzuri wa kitu huweza kuonekana kutoka nje tu; kwa kuangalia kisha kufanya uamuzi kuwa kitu hicho kinafaa.

Mkakasi ni mti mrefu ambao ni laini sana. Pia, ni chombo cha mviringo ambacho kina kifuniko na mle ndani kimezungushiwa mti. Mkakasi hupendeza sana kutoka nje lakini kilicho ndani ni kipande cha mti tu. Maana ya ndani ni kuwa usipumbazwe na umbo au sura ya kitu/mtu. Mtu ni tabia sio anavyoonekana kwa kumtazama tu. Upo uwezekano wa kitu kuvutia kutoka nje lakini kilicho ndani ni utupu usio na cha kuvutia au kutamanika.

Ukinzani unaopatikana hapa ni kuwa methali ya kwanza inatushawishi kutumia macho yetu kufanya uamuzi kulingana na tunachokiona kwamba kinatupendeza. Kwa upande wa pili, mkakasi hupendeza sana kwa kuutazama lakini ndani yake hakuna cha kupendeza. Je, iwapo kwa kutazama utamchagua nguruwe aliyenona kisha baada ya kumchinja tung’amue kuwa nyama yake haina utamu tuliotarajia, tutatukuwa tumefanya uamuzi mzuri? Kwa maoni yangu ni vyema zaidi kufanya uamuzi baada ya kufanya uchunguzi kwa undani pasipo kuongozwa na tunachokiona kutoka nje.

#### 4.8.1.3 Usimwamshe alalaye, ukimwamsha utalala wewe/ Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Neno ‘lala’ limebeba maana zaidi ya moja. Kwa kuzingatia maana ya juu ya methali ya kwanza, neno hili limetumika kumaanisha kuwa katika usingizi. Methali hii inatushauri kuwa tusijisumbue kukatiza usingizi wa huyu amepotezewa fahamu na usingizi au tutajipata wenyewe tumelala pia. Maana ya ndani ya methali hii inashauri kuwa sio jukumu letu kumsaidia jirani kujiondoa katika giza fulani. Unapokuwa umelala na kufunga macho, mazingira yako huwa yametawaliwa na giza. Kulingana

na methali hii, unaweza kuondoa giza hili kwa jirani na ujipate katika hali hiyo yake huku yeye akitamalaki katika mwangaza.

Methali ya pili nayo inatoa mwelekeo kwamba wakati ambao upo katika dhiki/tatizo au giza fulani, huwa unatarajia mtu akutue mzigo huo mzito unaokabiliana nao. Atakayekuondolea au kukusaidia kuondoa tatizo hili, huyo ndiye rafiki wako hata kama alikuwa adui wako hapo awali.

Ukinzani unaopatikana hapa ni kwamba methali ya kwanza inaelekeza jamii katika kutengana huku ya pili ikijaribu kuwaleta pamoja. Iwapo hutamsaidia jirani katika kupata suluhu ya changamoto anazokumbana nazo katika maisha yake ya kila siku, basi urafiki kati yenu hautakuwa umejengeka katika msingi na matarajio yafaayo. Kwa upande mwingine, ukizidi kumfaa mtu awe rafiki au hata adui wako, ni ishara tosha kwamba urafiki wenu unaendelea kudumishwa na umoja unajijenga. Mwanajamii ametwikwa jukumu la kuamua mwelekeo atakaofuata kwa kuzingatia methali hizi mbili ambazo zina mielekeo tofauti; utengano au umoja mtawalia.

### 4.8.2 Utambuzi wa Methali Kinzani Katika Fasihi ya Kiswahili.

Katika kiwango hiki, mtafiti alidhamiria kubaini iwapo wanafunzi wa vidato vilivyohusika katika utafiti huu wanatambua kuwepo kwa ukinzani katika methali za Kiswahili. Maoni haya aliyatoa kwa walimu kwani ndio wanaotoa mafunzo kwa wanafunzi wao na hatimaye kuwatahini ili kubaini uelewa wao. Walimu walitakiwa kutaja iwapo wanafunzi wao wanatambua kuwepo kwa methali kinzani katika lugha ya Kiswahili au la. Matokeo yako katika jedwali 4.19 lifuatalo:

**Jedwali 4.19: Utambuzi wa methali kinzani miongoni mwa wanafunzi**

| Utambuzi | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Ndio | 11 | 73.3 | 73.3 | 73.3 |
| La | 4 | 26.7 | 26.7 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **100** | |

Walimu walioshiriki walitoa majibu yanayodhihirisha kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wao wanatambua kuwepo kwa ukinzani katika methali. Asilimia 73.3 ni

ishara kwamba wanafunzi wengi wana uelewa wa methali kinzani huku asilimia 26.7 ikiashiria kwamba wapo wachache ambao hawana uelewa wa ukinzani ndani ya methali kinzani.

Idadi kubwa ya watafitiwa walikiri kuwa wanafunzi wao wana uelewa wa kuwepo kwa dhana ya ukinzani katika methali za Kiswahili. Ilibainika kwamba wengi wa walimu hawa wamefundisha dhana hii darasani na kwamba kutokana na mafundisho hayo wanafunzi wao wanazifahamu na wana uwezo wa kuzitaja na hata kutoa maana yake. Zaidi wanaweza kutoa mifano kutegemea muktadha wa mazungumzo au hata katika maandishi yao.

Asilimia 26.7 walisema kwamba wanafunzi wao hawana habari za kuwepo kwa methali kinzani katika fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya walimu walitoa maelezo kuwa wanafunzi wao hutumia methali za Kiswahili kwa ujumla kama tamathali ya usemi bila kuzingatia kuwa kuna methali nyingine inayokinzana na hiyo aliyotaja au la. Wengine walisema kuwa kwa wanafunzi wao, methali ni methali tu, bora iko katika muktadha fulani. Hii inatoa ishara kuwa wapo wanafunzi ambao hawatilii maanani maana inayotokana na tanzu za fasihi.

Kwa kulinganisha maoni ya watafitiwa kuhusu ufahamu wa methali kinzani, ni wanafunzi wachache tu ambao hawachukulii maana zinazotokana na fasihi simulizi kwa umakini unaofaa. Inawezekana kuwa baadhi ya wanafunzi wanaweza kutoa mifano ya methali zinazokinzana lakini wawe hawajawahi kukadiria kwa undani kuhusu suala la ukinzani. Kadhalika, utafiti huu ulibaini kuwa walimu wengi walioshiriki wamejikakamua vya kutosha na kuweza kufundisha darasani mada ya methali huku wakizingatia sifa za methali za Kiswahili.

### 4.8.3 Matumizi ya Methali Kinzani

Baada ya kubaini iwapo wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili wanatambua kuwepo kwa methali zenye maana kinzani, mtafiti alitaka kujua kama wanazitumia ipasavyo katika mazungumzo au maandishi. Matokeo yako katika jedwali 4.20 lifuatalo:

**Jedwali 4.20: Matumizi ya Methali Kinzani**

| Matumizi ya methali | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Ndio | 9 | 60 | 60 | 60 |
| La | 6 | 40 | 40 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **100** | |

Kutokana na utafiti huu ilibainika kuwa asilimia kubwa ya walimu wa fasihi ya Kiswahili walisema kuwa hata kama wanafunzi wao wana uelewa wa ukinzani katika methali za Kiswahili, hawazitumii methali hizi ipasavyo. Asilimia 60 ya watafitiwa walitoa maoni kuwa wanafunzi wao hawatumii methali katika mazingira yanayofaa huku asilimia 40 wakisema kuwa wanafunzi wao hutumia methali za Kiswahili ipasavyo.

Katika sehemu hii ya utafiti, watafiti walilenga kubaini iwapo wanafunzi hutumia methali kinzani ipasavyo. Kati ya walimu kumi na tano waliotafitiwa, walimu tisa walisema kuwa wanafunzi wao hutumia methali kinzani ipasavyo, kulingana na muktadha wa kimazungumzo na/au kimaandishi. Waliochukua mwelekeo huu walitoa sababu zao kuwa wanafunzi wao wanaelewa maana za methali na sifa zake kutegemea mazingira ya matumizi. Hii ni ishara tosha kwamba wanafunzi wengi ambao wamepata mafunzo kuhusu ukinzani wana uelewa tosha kuhusu matumizi ya methali za Kiswahili.

Walimu sita waliosema kuwa wanafunzi wao hawatumii methali kinzani ipasavyo walieleza kwamba wanafunzi wao hawana uelewa wa methali za Kiswahili kwa upana hivyo wanalemewa kuhusisha methali na muktadha. Watafitiwa wengine walisema kuwa baadhi ya wanafunzi wao hujikita tu katika matumizi ya methali kwa jumla bila kuzingatia ukinzani uliopo. Wanafunzi wengine hawana ufahamu wa ukinzani hivyo basi hujipata wakitumia methali moja kama tamathali ya usemi bila kuzingatia suala la ukinzani.

#### 4.8.4 Umuhimu wa Methali Kinzani Katika Fasihi ya Kiswahili.

Katika sehemu hii, mtafiti alilenga kubaini kutoka kwa watafitiwa iwapo kuna haja ya kuwa na methali zinazotoa maana zinazopingana katika fasihi ya Kiswahili. Watafitiwa walitarajiwa kuweka alama ya vema karibu na swali walilochagua kisha kutoa sababu ya jibu lao kwa kifupi. Jedwali 4.21 linaonyesha matokeo ya watafitiwa kuhusu umuhimu wa kuzidi kuwa na ukinzani katika methali za Kiswahili.

**Jedwali 4.21: Umuhimu wa Methali Kinzani Katika Fasihi ya Kiswahili.**

| Haja | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Ndio | 11 | 73.3 | 73.3 | 73.3 |
| La | 4 | 26.7 | 26.7 | 100 |
| **Jumla** | **15** | **100** | **100** | |

Mtafiti alitaka kujua kutoka kwa watafiti iwapo kuna umuhimu wa kuwa na methali zinazotoa maana kinyume katika fasihi ya Kiswahili. Matokeo yanabaini kuwa asilimia kubwa ya walimu waliotafitiwa wanaonelea kuwa methali kinzani zina nafasi katika fasihi ya Kiswahili. Asilimia 73.3 wanasema kwamba kuna umuhimu wa kuwa na methali kinzani huku asilimia 26.7 wakisema kwamba hakuna haja ya kuwa na methali kinzani.

Asilimia kubwa ya watafitiwa walisema kuna haja ya kuwa na methali kinzani katika fasihi ya Kiswahili. Kulingana nao, methali hutoa mafunzo yanayofaidi jamii ikizingatiwa kwamba kila methali ina maana kwa hadhira. Aidha, methali hizi hutumika na jamii kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika shughuli zao za kila siku. Methali hutoa suluhu kuhusu mambo tofauti. Kadhalika, maisha ya kawaida ya mwanadamu yamejaa hali ya ubishi na unyume. Maishani tunakutana na watu wajinga/werevu, wazembe/wenye bidii. Katika hali kama hii, methali kinzani hutoa mwelekeo kutegemea hali unayokabiliana nayo kama mwanajamii. Ukinzani katika methali za Kiswahili upo kuhakikisha kuwa zinatoa mwelekeo fulani na unaofaa kulingana na hali mahususi. Methali fulani huwakilisha hali fulani katika jamii.

Watafitiwa waliochukua msimamo wa kukosa imani na methali kinzani walisema kwamba ukinzani katika methali huleta utata kimaana na kimatumizi. Walichokisisitizia ni kuwa hawapati umuhimu wa kuwa na methali ambazo zinatoa

maana zinazokinzana. Huku ni kupoteza maana katika fasihi ambapo inapaswa kutoa mwelekeo fulani. Wakati methali imetoa mwelekeo fulani kisha nyingine inatoa maana iliyo kinyume, basi kulingana nao tamathali hii ya usemi haina umoja. Kwa mfano, '*chelewa chelewa utapata mwana si wako'* na mwingine akwambie *'simba mwenda mpole ndiye mla nyama'*. Katika hali kama hii methali haijatoa mwelekeo bali imekupa mawaidha kama mwanajamii uamue njia utakayoifuata; methali hizi hazitakupa suluhu kama mwanajamii.

### 4.8.5 Changamoto katika Ufundishaji wa methali kinzani darasani.

Mtafiti alidhamiria kubaini iwapo walimu wanapitia changamoto fulani wanapotoa mafunzo ya methali zenye maana kinyume kwa wanafunzi wao. Kila mtafitiwa alitarajiwa kutaja baadhi ya changamoto ambazo anazipitia kama mwalimu wa fasihi ya Kiswahili haswa anapotoa ufafanuzi wa maana za methali zinazokinzana. Matokeo yako katika jedwali 4.22 lifuatalo:

**Jedwali 4.22: Changamoto za kufundisha ukinzani katika methali za Kiswahili**

| Changamoto | Idadi | Asilimia | Asilimia Halisi | Asilimia Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| Ndio | 15 | 100 | 100 | 100 |
| La | 0 | 0 | 0 | |
| Jumla | 15 | 100 | 100 | 100 |

Baada ya kukusanya data kutoka kwa walimu wa fasihi ya kidato cha tatu na cha nne, ilibainika kwamba kuna changamoto kubwa kwa walimu wanapojadili suala la methali zilizo na ukinzani. Asilimia 100 ya walimu waliotafitiwa walikiri kwamba wanafunzi wao wanakosa kuelewa sababu ya kuwepo kwa methali moja inayotoa mwelekeo fulani kisha nyingine inajitokeza na kutoa maana iliyo kinyume kabisa na ile ya kwanza. Hili ni tatizo katika fasihi ya Kiswahili linalohitaji utafiti wa kina.


Watafitiwa wote walioshiriki katika zoezi hili walikiri kuwa kuna changamoto wanapofundisha ukinzani kama mojawapo ya sifa za methali za Kiswahili. Kupata asilimia 100 ya walimu wakikabiliana na matatizo wanapojadiliana na wanafunzi kuhusu ukinzani, ni ishara tosha kuwa suluhu inahitajika. Baadhi ya wanafunzi hukabiliana na tatizo la kubaini ni methali gani inayosema ukweli kati ya jozi fulani

ya methali zinazokinzana. Changamoto hii hujidhihirisha kutokana na maswali wanayozua wanafunzi, kuhusu tofauti ya maana na matumizi ya methali kinzani. Wanafunzi wengine hupata tatizo kubwa kuelezea namna ukinzani unavyojitokeza katika methali. Hili linaweza kutokana na hali ya baadhi yao ya kutofahamiana na kutoingiliana sana na methali za Kiswahili. Hivyo basi, wengi wao huonekana kukosa imani na ukinzani huu kwani hawaoni sababu ya kuwepo na methali zinazoleta maana zinazokinzana. Aidha, kutomakinika kwa wanafunzi huchangia katika kuwasababishia kukanganyikiwa zaidi. Waliotoa changamoto hii walielezea kuwa wapo wanafunzi ambao kwao methali inapaswa kutoa mwelekeo. Hata hivyo, wengi hutumia nafasi hii kuzua ubishi hivi kwamba ukitumia methali moja kumpa mwelekeo au wosia, naye atakupa nyingine inayotoa maana kinyume na uliyomsemea. Hali kama hii hupatikana miongoni mwa wanafunzi walio na ufahamu wa methali na sifa zake kwa undani.

### 4.8.6 Mielekeo ya Walimu Kuhusu Ukinzani wa Methali

Lengo la latu la utafiti huu lilikuwa kubaini na kuchanganua mielekeo ya walimu kuhusu methali zilizo na maana kinzani. Kila mwalimu alitarajiwa kutaja mwelekeo wake; chanya au hasi na kutoa sababu za kuchukua mwelekeo huo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyeshwa katika jedwali 4.23 lifuatalo na kuchanganuliwa na mtafiti:

**Jedwali 4.23: Mielekeo wa Walimu Kuhusu Ukinzani wa Methali**



Kutokana na data iliyokusanywa kutoka kwa walimu wa fasihi ya Kiswahili, ni wazi kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa wana mwelekeo chanya kuhusu suala la ukinzani katika methali za Kiswahili. Asilimia 66.7 ya watafitiwa ni ya walio na mwelekeo chanya huku asilimia 33.3 ikiwa ya walio na mwelekeo hasi.

Watafitiwa waliochagua mwelekeo chanya walisema kuwa methali za Kiswahili zinakinzana kimaana lakini kila methali ikitumika katika muktadha wake basi ukinzani huu hauleti mwelekeo hasi. Walisisitiza kwamba ukinzani humpa mtumiaji lugha uwezo wa kuchagua methali moja kulingana na muktadha au hali fulani huku akipuuza ile ambayo inatoa maana kinyume hivi kwamba ikitumiwa italeta madhara unapochagua mwelekeo unaotaka kufuata. Wengine walionelea kwamba methali kinzani huwakilisha maisha halisi ya binadamu ambayo yamejaa ukinzani; upendo/chuki, ujinga/-erevu na kadhalika.

Waliosema kwamba ukinzani katika methali za Kiswahili huleta mwelekeo hasi walitoa sababu zao na kusema kuwa ukinzani huleta utata kimatumizi na kimaana. Kadhalika, walisema kuwa methali zinazotoa maana kinyume humweka mtumiaji lugha katika hali ya kuchanganyikiwa hivi kwamba asijue ni methali gani atakayochagua na impe mwelekeo unaofaa na ni gani atakayopuuza.

Kipacha (2014) anatoa madai kwamba katika siku za hivi karibuni, watumiaji lugha wamekuwa wakizipinda methali kimakusudi ili kuleta dhihaka ambayo ina uhalisi na ukweli. Mfano anaotoa ni ule wa methali *mvumilivu hula mbivu* ambayo ilipinduliwa na Mochiwa (1988) na kuwa *mvumilivu hula mbovu*. Upindwaji huu unaweza kujitokeza kama njia ya kuleta dhihaka lakini tukizingatia maana yake, ni methali ambayo imebeba ujumbe mzito na unaoshinikizia mabadiliko miongoni mwa wanajamii. Kwa kweli methali hii ina maana sawa na methali, *chelewa chelewa utapata mwana si wako.*

Kutokana na maoni ya watafitiwa, ukinzani katika methali unaleta mwelekeo chanya miongoni mwa watumiaji lugha ya Kiswahili. Kutokana na utafiti, idadi kubwa ya watafitiwa walikubaliana na kauli hii. Walitetea msimamo wao na kusema kuwa methali ikitumiwa katika mazingira yanayofaa itatoa mwongozo kwa anayekabiliana na hali fulani. Hata hivyo, utata wa kimaana na kimatumizi ni jambo lingine lililozuka

kwa uwazi kwa sababu methali hizi zipo, hatuwezi kuzipuuza. Kila moja ina maana yake lakini zinapotoa maana kinyume, ni gani ambayo inapeana mwelekeo unaofaa? Ni gani ya kufuatwa na ni gani itakayotwezwa? Haya ni baadhi ya maswali yaliyozuliwa na watafitiwa walio na mwelekeo hasi kuhusu methali kinzani.

# SURA YA TANO

# MUKHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inayokamilisha utafiti huu imebeba mukhtasari wa kazi nzima ya utafiti. Aidha, utafiti huu umetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye zinazohusiana na suala la ukinzani katika methali kwa watafiti na wasomi wa fasihi ya Kiswahili. Hatimaye, mtafiti atatoa hitimisho kuhusu utafiti huu.

## 5.2 Mukhtasari wa Matokeo

Utafiti huu umeangazia suala la ukinzani na mielekeo ya jamii kuhusu ubishi unaopatikana katika methali za Kiswahili. Tulitathmini mielekeo ya wanafunzi wa fasihi kutoka kidato cha tatu na cha nne na pia tukachanganua maoni ya walimu wa fasihi ya Kiswahili kuhusu ukinzani katika methali za Kiswahili. Katika uchanganuzi wetu, tulitumia nadharia mbili; ya umaanishaji na nadharia ya mguso. Malengo yaliyoongoza katika ufanikishaji wa utafiti huu ni yafuatayo:

1. Kubainisha mielekeo ya wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne kuhusu methali zenye ukinzani.
2. Kutathmini mielekeo ya wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne kwa kutumia kigezo cha uchanya na uhasi.
3. Kuchanganua mielekeo ya walimu kama waelekezi na watahini wa somo la fasihi ya Kiswahili kuhusu ukinzani katika methali za Kiswahili.

Kwa kuzingatia lengo la kwanza la utafiti huu, ilibainika wazi kwamba wanafunzi katika eneo lililohusika katika utafiti huu wana mielekeo tofauti kuhusu suala la ukinzani wa methali za Kiswahili. Mtafiti aliongozwa na lengo la pili ambapo alitumia vigezo vya uchanya na uhasi ili kubaini msimamo mahususi wa kila mtafitiwa. Matokeo yalidhihirisha kuwa asilimia 53 walikuwa na mwelekeo chanya huku asilimia 47 wakiwa na mwelekeo hasi kuhusu ukinzani. Walioegemea upande wa uchanya walitoa msimamo kwamba ukinzani wa methali ni ishara tosha ya namna maisha ya kawaida yalivyo na ukinzani wa hali; kila methali iliyo na maana kinyume inawakilisha hali halisi. Waliogemea upande wa uhasi walitetea msimamo wao kwa kutoa madai kwamba methali kinzani huleta utata wa kimaana na kimatumizi.

Wengine walitoa maoni kwamba ni vigumu kutumia methali zilizo na ukinzani kutoa mwelekeo kwa wanajamii kwani utamsemea methali moja naye atakutajia methali nyingine inayotoa maana kinyume na uliyotaja hapo awali.

Lengo la tatu la utafiti huu liliwalenga walimu wa fasihi ya Kiswahili katika vidato vya tatu na nne. Mtafiti alitumia vigezo vya uchanya na uhasi kubainisha kwa urahisi mwelekeo wa kila mwalimu aliyehusika katika utafiti huu. Asilimia 66.7 walisema kuwa ubishi katika methali za Kiswahili unaleta mwelekeo chanya huku asilimia 33.3 wakisema ubishi huu huleta mwelekeo hasi. Walioegemea upande wa uchanya walitetea msimamo wao kwa kusema kuwa methali hukinzana tu kimaana lakini kila methali ikitumika katika muktadha unaofaa, ukinzani haupo tena. Kila methali ina maana na matumizi yake. Kwa upande mwingine, Walioegemea upande wa uhasi walitoa maoni kwamba ukinzani katika methali huleta utata na kuchanganyikiwa kwingi hivi kwamba mtumiaji lugha atashindwa kufanya uamuzi wa ni methali gani atakayoichagua ili impe mwelekeo unaofaa.

Utafiti huu umedhihirisha wazi kwamba jamii inaelewa na kukumbatia kuwepo kwa methali zilizo na maana kinzani katika fasihi ya Kiswahili.  Idadi kubwa ya watafitiwa wakiwemo wanafunzi na walimu wao wa fasihi wana mwelekeo chanya kuhusu ubishi huu katika methali za Kiswahili. Kilichodhihirika hapa ni kwamba methali kinzani zinawakilisha ipasavyo maisha kinzani ya jamii yetu. Katika jamii kuna watu na hali zinazokinzana; kuna urafiki/uadui, mapenzi/chuki, uzembe/uvivu, ujinga/werevu na kadhalika. Uhalisia huu ulio na pande mbili, unawakilishwa na methali ambazo hutoa maana au miongozo inayowakilisha kila upande. Kinachopaswa kuzingatiwa ni iwapo methali utakayochagua kufuata ukiwa katika hali fulani itakuwa inakupeleka kuliko kwema ama itakuwa ya kukupotosha tu.

## 5.3 Hitimisho

Kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti, mambo yafuatayo yaliweza kudhihirika:

1. Wanafunzi tofauti wana mielekeo inayotofautiana kuhusu suala nzima la ukinzani katika methali za Kiswahili.
2. Baada ya kufasili matokeo ya utafiti, wanafunzi wengi (asilimia 53) wana mwelekeo chanya kuhusu ukinzani unaopatikana katika methali za Kiswahili.

3. Walimu wa fasihi ya Kiswahili waliohusika katika utafiti walidhihirisha kwamba wanakumbatia ukinzani katika methali za Kiswahili.

Kilichotiliwa mkazo katika utafiti huu ni ile maana inayopatikana katika methali fulani. Hata hivyo, kuna wanajamii ambao kwa maoni yao ukinzani katika methali za Kiswahili haupaswi kuwa katika fasihi kwani unaleta utata wa maana na matumizi.

**5.4 Mapendekezo**

Utafiti huu ulijifunga katika utanzu wa fasihi simulizi, hususani semi ya methali za Kiswahili. Tatizo la utafiti katika kazi hii lilikuwa kubaini mielekeo ya watumiaji lugha kuhusu suala la methali zinazotoa maana zilizo kinyume. Kufanikisha hili, mtafiti alijifunga katika nadharia mbili; ya umaanishaji na nadharia ya mguso ambazo mihimili yao kuu iko katika maana inayoletwa na fasihi na athari au mguso unaoletwa na fasihi mahususi, mtawalia.

Ili kuwezesha methali za Kiswahili kuzidi kutumika kama chombo madhubuti cha kutoa mwongozo kwa wanajamii, kuna baadhi ya mambo yanayopaswa kutekelezwa yakiwemo:

1. Katika somo la Kiswahili kwenye shule za upili kuwekwe uzito mahususi wa vipengele vya fasihi simulizi. Hili litajuimuisha namna fasihi simulizi, hususani methali zinavyofundishwa shuleni. Utafiti huu ulibaini kwamba wanafunzi wengi wana uelewa wa kiwango cha chini sana kuhusu suala la ukinzani wa methali za Kiswahili. Sifa hii inapaswa ipewe uzito unaofaa.

2. Kwa kadri ipasavyo, matumizi ya methali za Kiswahili yapewe nafasi kubwa katika mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hili linaweza kufikiwa wakati wa kuidhinisha sera kuhusu lugha ya kutumiwa shuleni. Shule nyingi hujivunia kutumia lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi na lugha ya mawasiliano shuleni huku zikikatiza kabisa matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Fasihi ya Kiswahili ni uwanja mpana sana wa utafiti. Wasomi wengi wa fasihi wametafitia kwa upana mno fasihi andishi. Kimsingi aina hizi mbili za fasihi hutegemeana na kurutubishana. Hivyo basi, ipo haja ya kufanya tafiti kuhusu utanzu

wa fasihi simulizi. Utafiti huu unapendekeza kuwa, tafiti zaidi zinaweza kufanywa kuhusu mambo yafuatayo;

Kwanza, tafiti tofauti zifanywe kuhusu ukinzani wa methali katika lugha tofauti za kikabila au za kiafrika. Kila lugha ina semi hususani methali zikiwa mojawapo wa tanzu za fasihi simulizi. Semi hizi huwa na uhusiano wa karibu sana na mazingira ambapo lugha fulani hutumika. Kutokana na dai hili, katika fasihi hizi kuna methali zinazotoa maana kinyume.

Pili, utafiti unaweza ukafanywa kuhusu mielekeo ya ukinzani wa methali za Kiswahili ambapo uchunguzi unapaswa kufanywa kwa watafitiwa wazee (walio na miaka 60 na zaidi) haswa wale ambao asili yao ni ya pwani ambapo Kiswahili kimekita mizizi. Utafiti huo utakuwa tofauti na huu kwani watafitiwa na eneo la utafiti sio sawa. Matokeo ya tafiti hizi mbili yatakuwa tofauti sana.

# MAREJELEO


Abdu, M. (1978). *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Andrzejewski, B. W., Pilaszewicz, S., & Tyloch, W. (Eds.). (1985). *Literatures in African languages: theoretical issues and sample surveys*. Cambridge University Press.

Chinua, A. (1959). *Things fall apart*. Nigeria: Heinemann Ltd.

Felician, A. (2017). *Kuchunguza Ujinsia na Matumizi ya Lugha katika Methali za Wakurya* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Gergen, K. J. (1990). *Proverbs, pragmatics, and prediction*. Canadian Psychology, 31, 212-214.

Grace, G. (Ed.). (2013). *Education and the City: Theory, History and Contemporary Practice.* Routledge

Grice, H. P. (1975). *"Logic and Conversation."*In: Cole, P. & Morgan, 1. (Eds.), *Syntax and Semantics* (pp. 41-58). New York: Academic Press.

John C.N. (2011). *Dokezo za Sitiari Katika Methali za Kiswahili na Kiganda* (Doctoral dissertation. Makerere University).

Kalugia L. & Lodhi A. Y. (1980).*Methali Zaidi za Kiswahili Kutoka Afrika Mashariki*. Uppsala: Scandinavian Institute of African Studies.

Kanu A. (2014). *Igbo Proverbs as Embodiments of Igbo-African Philosophy.* International Journal of Humanities and Social Science *Vol.* 4 *No.1; pg 164*-168

King'ei, K. G. & Ndalu, A. E. (1989). *Kamusi ya methali za Kiswahili*. East African Publishers.

Kipacha, A. (2014). *Misemo katika lugha za Magari: Divai mpya?* In Swahili Forum (Vol. 21).

Kothari, C.R. (2004) *Research Methodology: Methods and Techniques (2nd edition.)* New Delhi: New Age International (P) Ltd. Publishers.

Madumulla, J. S. (1995). *Proverbs and sayings*. *Theory and Practice*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mazrui, A. M & Syambo, B.K. (1992).*Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mhando, P na Balisidya,N. (1976). *Fasihi na sanaa za maonyesho.* T.P.H. Dar es Salaam.

Mieder, W. (2007). *Proverbs as cultural units or items of folklore*., Phraseology: An international handbook of contemporary research (pp. 394-414). Berlin, Germany:

Mieder, W. & Litovkina, T. (1999). *Twisted wisdom: modern anti- proverbs (vol. 4).* University of Vermont.

Mkota, A. (2009). *Kamusi ya methali: maana na matumizi*. Vide-Muwa Publishers.

Mochiwa, Z. (1988). *Mvumilivu hula mbovu*. Dar es Salaam University Press.

Mtesigwa, G. K. (2013). *Kuchunguza Matumizi ya Methali katika Jamii ya Wanyiramba (Doctoral dissertation*, The Open University of Tanzania).

Mugenda O.M na Mugenda A.G. (2012). *Research Methods Dictionary*. Nairobi: Applied Research & Training services.

Mulokozi, M.M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi.* Dar es Salaam: TUKI.

Murithi, M.M. (2015). *Uchanganuzi wa Methali za Kiswahili: Mtazamo wa Kiudenguzi* (Doctoral dissertation, Kenyatta University).

Nestor, H. B. (1977). *500 proverbs (Haya): methali, emigani*. East African Literature Bureau.

Ngole, S. A & Honero, L.N. (2004). *Fasihi – Simulizi: Methali.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta foundation

Orodho, A. J. (2003). *Essentials of educational and social science research methods*. Nairobi: Masola Publishers.

Oxford University Press na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili)

Sito, P. S. (2015). *Athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati: mfano wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Taylor, R. (1981). *Understanding the Elements of Literature*. London: Macmillan

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press: East Africa Ltd. Kenya

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press: East Africa Ltd. Kenya

Vasquez, A.S. (1973). *Art and Society*. New York: Monthly Review Press.

Wamitila, K.W. (2001). *Kamusi ya methali*. Lulu za Lugha 2. Nairobi Longhorn Publishers.Vol. 2.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. English Press, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi* (Vol. 1). Vide-Muwa Publishers.

Wellek, R. W. (1949). *Theory of Literature*. New York: Harvest.

Wellek, R.W. & Warren, A. (1963). *Theory of Literature.* 1949. New York, 3, 255-257.

Yankah, K. (1989). *The Proverb in the Context of Akan Rhetoric.* New York: Peter Lang Publishing

Yankah, K. (1994). *Do proverbs contradict? Wise Words*, 127- 41.New York: Peter Lang Publishing

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho I:** Hojaji kwa Wanafunzi

**Mielekeo ya Wanafunzi wa Shule za Upili Kuhusu Methali Kinzani Katika Kata ya Kitui Mjini; Kaunti ya Kitui; Kenya.**

Hojaji hii ililenga kukusanya data kutoka kwa wanafunzi wa shule za upili, kidato cha tatu na cha nne. Data hii ilisaidia kubaini mielekeo ya wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili kuhusu methali kinzani.

Tafadhali weka alama ya vema ***(tick)*** karibu na jibu utakalochagua kuwa sahihi. Usiandike jina lako popote kwenye hojaji hii.

**SEHEMU YA KWANZA:HABARI YA KIBINAFSI:**

1. Taja jinsia yako:

   Kiume ☐

   Kike ☐

2. Taja kidato chako:

   Kidato cha 3 ☐

   Kidato cha 4 ☐

**SEHEMU YA PILI: MASWALI YANAYOHUSIANA NA UTAFITI**

**3.** Eleza ukinzani unaopatikana katika jozi za methali zifuatazo:

(i) *Adui mpende/ Anipendaye nampenda, anikaataye nami namkataa*-------
---------------------------------------------------------------------------------
-------------------------

(ii) *Mwenye shoka hakosi kuni/ Penye miti hapana wajenzi* ------------------
---------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------
-----------------------------------------------------

(iii) *Nahodha wengi chombo huenda mrama/ Panapo wengi hapaharibiki jambo*---------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------

(iv) *Fuata nyuki ule asali/ Fuata nyuki ufie mzingani* -------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------

(v) *Akutendeaye ubaya, mlipe kwa wema/ Akutendaye mtende*---------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------

*(vi)* *Mavi ya kale hayanuki/ Mavi ya kale hayaachi kunuka* -------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------

*(vii)* *Ngoja ngoja huumiza matumbo/ Mstahimilivu hula mbivu* ---------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------

*(viii)* *Adhihakiye kovu hajaona jeraha /Achekaye kilema hata kwao kipo*-----

-------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------

4. Kwa kuzingatia jozi za methali zifuatazo, ungependelea methali gani itumike katika jamii? Elezea jibu lako.

   (i) *Adui mpende / Anipendaye nampenda, anikaataye nami namkata* -------------------------------------------------------------

   ---------------------------------------------------------------------------

   ----------------------------------------

   (ii) *Mwenye shoka hakosi kuni/ Penye miti hapana wajen* ------

   ---------------------------------------------------------------------------

   ---------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------

   (iii) *Nahodha wengi chombo huenda mrama / Panapo wengi hapaharibiki jambo*-----------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
---------------------------------

(iv) *Akutendeaye ubaya, mlipe kwa wema* ☐ */ Akutendaye mtende* ☐
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
----------------------------------

(v) *Fuata nyuki ule asali* ☐ */ Fuata nyuki ufie mzingani* ☐----------
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------

(vi) *Mavi ya kale hayanuki* ☐ */Mavi ya kale hayaachi kunuka* ☐----
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------

(vii) *Ngoja ngoja huumiza matumbo* ☐ */ Mstahimilivu hula mbivu* ☐
--------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
---------------------------------

(viii) *Adhihakiye kovu hajaona jeraha* ☐ */ Achekaye kilema hata* ☐ *kwao kipo* ------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------

5. Taja mifano ya jozi za methali za Kiswahili zilizo na ukinzani:

(i) ----------------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------------------------

(ii) ----------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------

(iii) ----------------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------------------------

(iv) ----------------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------------------------

6. Kuna haja ya kuwa na methali kinzani katika lugha ya Kiswahili? (i) Ndio ☐ ☐
(ii)La

Elezea jibu lako--------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------

7. Ukinzani katika methali za Kiswahili huleta mwelekeo (i) Chanya ☐ (ii) Hasi ☐

Elezea jibu lako--------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------
----------------------------------------------

**NASHUKURU KWA MSAADA WAKO**

**Kiambatisho II: Hojaji kwa Walimu**

**Mielekeo ya Wanafunzi wa Shule za Upili Kuhusu Methali Kinzani Katika Kata ya Kitui Mjini; Kaunti ya Kitui; Kenya.**

Hojaji hii ililenga kukusanya data kutoka kwa walimu wa Fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu ulidhamiria kubaini mielekeo ya watumiaji wa methali kuhusu ukinzani wa methali katika lugha ya Kiswahili. Maswali katika hojaji hii yaliongoza katika kufikia na kutathmini lengo hili.

Tafadhali weka alama ya vema (tick) karibu na jibu utakalochagua kuwa sahihi. Usiandike jina lako popote kwenye hojaji hii.

**<u>SEHEMU YAKWANZA: MAELEZO YAKO BINAFSI:</u>**

1) Taja jinsia yako

   Kiume ☐

   Kike ☐

2) Umefunza Fasihi ya Kiswahili jumla ya miaka ngapi?

   Miaka 15 na zaidi ☐

   Miaka 10 – Miaka 15 ☐

   Miaka 5- Miaka 10 ☐

   Miaka 0 – Miaka 5 ☐

3) Unafunza Fasihi ya Kiswahili kidato kipi?

   Kidato cha 3 ☐

   Kidato cha 4 ☐

4) Je, wewe ni mtahini wa Fasihi ya Kiswahili?

   Ndio ☐

   La ☐

**<u>SEHEMU YA PILI: MASWALI YANAYOHUSIANA NA UTAFITI</u>**

7. Taja mifano ya jozi za methali za Kiswahili zilizo na ukinzani:

   (i) ------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------

   -------------------------------------------------------

(ii) -------------------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------

(iii) -------------------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------

(iv) -------------------------------------------------------------------------------------
-------------------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------

8. Wanafunzi wako wanatambua kuwepo kwa methali kinzani katika lugha ya Kiswahili?

   Ndio ☐

   La ☐

   Eleza.-----------------------------------------------------------------------------------
   ---------------------------------------------------------------------------------------------
   ---------------------------------------------------------------------------------------------
   -----------------

9. Wanafunzi hawa hutumia methali kinzani ipasavyo?--------------------------------
   ---------------------------------------------------------------------------------------------
   ---------------------------------------------------------------------------------------------
   ---------------------------------------------------------------------------------------------
   -----------------

10. Kwa maoni yako, upo umuhimu wa kuwa na methali kinzani katika lugha ya Kiswahili? -------

    Eleza------------------------------------------------------------------------------------
    ---------------------------------------------------------------------------------------------
    ---------------------------------------------------------------------------------------------
    ---------------------------------------------------------------------------------------------
    -----------------

11. Kama mwalimu wa fasihi ya Kiswahili unapitia changamoto zipi unapofafanua maana na matumizi ya methali hizi kwa wanafunzi wako --------
    ---------------------------------------------------------------------------------------------
    ---------------------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------

12. Ukinzani katika methali unakupa mwelekeo upi kama mtumiaji wa lugha ya Kiswahili? -----------

----------------------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------

**NASHUKURU KWA MSAADA WAKO**

## Kiambatisho III: Ratiba ya Kazi

| KAZI | MWEZI | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | NOV '17 | DEC 17- MAR 18 | | | | APR | MAY | JUN | JUL | AUG | SEP | OCT | NOV | DEC |
| Kutafuta mada ya utafiti | | | | | | | | | | | | | | |
| Kuandika pendekezo | | | | | | | | | | | | | | |
| Kutetea pendekezo la utafiti | | | | | | | | | | | | | | |
| Kukusanya data | | | | | | | | | | | | | | |
| Kuchanganua data | | | | | | | | | | | | | | |
| Kuandika Ripoti | | | | | | | | | | | | | | |
| Kutetea na kuandika ripoti ya mwisho | | | | | | | | | | | | | | |
| Kuchapisha nakala | | | | | | | | | | | | | | |

## Kiambatisho IV: Bajeti

| **BIDHAA** | **KIASI** | **GHARAMA** | **GHARAMA YA JUMLA** |
|---|---|---|---|
| HOJAJI | 90 | 20 | 1,800 |
| PENDEKEZO | 4 | 400 | 1,600 |
| TASNIFU | 9 | 2,500 | 22,500 |
| VITABU | 3 | 200 | 600 |
| KALAMU | 5 | 20 | 100 |
| NAULI | - | - | 18,000 |
| RAMANI | 1 | 3,000 | 3,000 |
| DISKI MWEKO | 1 | 2,500 | 2,500 |
| MATUMIZI YA ZIADA | - | 25,000 | 25,000 |
| **JUMLA** | | | **75,100** |

## Kiambatanisho III: Orodha ya Shule za Upili Eneo Bunge la Kitui Mjini

1. Shule ya wavulana ya Kitui.
2. Shule ya mseto ya Muslim.
3. Shule ya wavulana ya St. Charles Lwanga.
4. Shule ya mseto ya Ivaini.
5. Shule ya wasichana ya St. Ursula Tungutu.
6. Shule ya mseto ya Kaveta St. Stephen.
7. Shule ya mseto ya Kwa -Ngindu.
8. Shule ya mseto ya Katyethoka.
9. Shule ya mseto ya Mutendea.
10. Shule ya mseto ya Kwa- Ukungu.
11. Shule ya mseto ya Mbusyani.
12. Shule ya mseto ya Ngiini.
13. Shule ya mseto ya Engineer Ngilu.